SportPesa
CHEZA USHINDE SASA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



**Aliyemuua** mama yake mbaroni kwa tuhuma kumuua, kumfukia mke wake

UKURASA 8



CAMEROON YAPEWA BRAZIL, TUNISIA KUIVAA UFARANSA

UKURASA 21

Nipashe
JUMAPILI
MWANGA WA JAMII
Jumapili Aprili 3, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
www.ippmedia.com
ISSN 0856 • No. 0580904
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



# Samia amulika nidhamu ya woga

- **Aanika** sababu mawaziri kubadilishwa
- **Asisitiza** hatafoka, lakini kalamu... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

**SERIKALI KUWEKEZA ZAIDI KWENYE SEKTA UZALISHAJI**

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, ameliambia Shirika la Mpango...

UKURASA WA 5

**MAASKOFU WASTAAFU KKKT WAPEWA SOMO**

MAASKOFU wastaafu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) nchini...





Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akikabidhi Mwenge wa Uhuru kwa Kiongozi wa mbio za Mwenge kitaifa kwa mwaka 2022, Tahili Nyandabara, baada ya kuuwasha na kuzindua mbio hizo, katika Uwanja wa Sabasaba, mkoani Njombe jana. **PICHA: OMR**

## Mbio Mwenge kutia mkazo mambo saba kwa siku 195


UKURASA 2

RIPOTI MAALUMU

## Risasi iliyomuua mwanakijiji mgodini inavyozua mtafaruku

UKURASA 4

**MICHEZO** SIMBA KUSUKA AU KUNYOA LEO UK.24 | **MAONI, KATUNI** UK.6



Viongozi walioapishwa na Rais Samia Suluhu Hassan (kutoka kulia), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge, Sera na Uratibu, George Simbachawene, Waziri wa Katiba na Sheria, Damas Ndumbaro, Waziri wa Maliasili na Utalii, Pindi Chana, Mwenyekiti wa Baraza la Maadili, Jaji mstaafu Ibrahim Mipawa, Wajumbe wa Baraza hilo, Peter Ilomo na Suzan Mlawi, wakila kiapo cha maadili, kilichoongozwa na Kamishna wa Maadili, Jaji Sivangilwa Mwangesi, Ikulu Chamwino mkoani Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

# Mwenge kumulika mambo 7 siku 195

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MAKAMU wa Rais wa Tanzania, Dk. Philip Mpango, amezindua rasmi mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka huu, akiagiza mambo saba yanayotakiwa kutiliwa mkazo.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa mbio hizo kwenye viwanja vya Sabasaba mjini Njombe jana, Dk. Mpango aliwataka waratibu wote wa Sensa ya Watu na Makazi nchini kuwaandaa wananchi ili washiriki kikamilifu wakati wa sensa hiyo miezi minne ijayo.

Alisema viongozi hao wanatakiwa kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa sensa sambamba na miongozo na taratibu zitakazofanikisha sensa kwa ufanisi.

Makamu wa Rais aliwataka viongozi wa siasa, dini na mashirika yasiyo ya kiserikali kuelimisha na kuhamasisha wafuasi wao kuhesabiwa Agosti mwaka huu.

Dk. Mpango alisema kuwa kupitia mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka huu, wananchi wote wana jukumu la kupambana na rushwa chini ya kaulimbiu inayosema 'Kupambana na rushwa ni jukumu langu'.

"Nitumie nafasi hii kuwakumbusha TAKUKURU (Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa) kutekeleza agizo la Rais Samia Suluhu Hassan kukamilisha uchunguzi wa miradi 52 iliyotiliwa shaka wakati wa mbio za Mwenge mwaka jana.

Aliwataka waliopewa dhamana ya kukimbiza Mwenge kuhakikisha wanajiridhisha na kufungua miradi ambayo inalingana na thamani ya fedha zilizotumika.

Dk. Mpango, akizungumzia jambo la tatu ambalo ni maambukizi ya Virusi vya Ukimwi, alisema vijana ambao ndiyo nguvu kazi ya taifa, ndiyo wanaonekana kuathirika zaidi na janga hilo.

"Utafiti wa mwisho wa viashiria na matokeo ya Ukimwi hapa nchini ulifanyika ngazi ya kaya mwaka 2016/17 na ulionyesha kuwa mikoa iliyokuwa na maambukizi ya juu ya Ukimwi ni pamoja na Njombe ambao ulikuwa na maambukizi kwa asilimia 11.4," alisema.

Dk. Mpango pia alisema wananchi wanapaswa kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa wa malaria kwa kuwa una athari kubwa ikiwamo vifo vingi hasa kwa watoto chini ya umri wa miaka mitano, pia mama wajawazito, wazee na vijana.

Makamu wa Rais alisema nguvu pia inahitajika katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya, akiagiza Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya iendelee na operesheni kwenye mipaka ya ndani na nje ya nchi na watakaobainika wakamatwe kwa sababu wanaharibu nguvu kazi ya taifa.

Dk. Mpango pia alisisitiza suala la lishe ambalo bado ni tatizo kubwa kiafya kutokana na ukosefu wa lishe bora kwa wananchi.

"Kila binadamu anatakiwa kula chakula bora na cha kutosha chenye virutubisho vyote vinavyohitajika ukijumlisha vyakula vya asili ya nafaka, mizizi na ndizi jamii ya kunde mboga, bila ya kusahau maji safi na salama vikiambatana na mazoezi ya mwili ambayo ni msingi wa afya njema," alisisitiza.

Makamu wa Rais pia aliwataka Watanzania kupunguza matumizi ya pombe, vileo, sigara na bidhaa nyingine za tumbaku na kuepuka kutumia dawa za kulevya.

Pia alisisitiza suala uhifadhi na utunzaji wa mazingira kama moja ya vipaumbele muhimu vya serikali ya awamu ya sita.

Awali Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) Prof. Joyce Ndalichako, alisema Mwenge wa Uhuru utakimbizwa kwa siku 195 katika mikoa yote 31 na halmashauri zote 195 za Tanzania.

"Kazi hii itafanywa na vijana sita kutoka Tanzania Bara na Visiwani ambao watatambulishwa kwako," alisema Prof. Ndalichako.

Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Waziri Kindamba, alisema uamuzi wa serikali kuchagua Mkoa wa Njombe kuzindua mbio za Mwenge kitaifa mwaka huu umefanyika akati mwafaka kwa kuwa ni mkoa huo unaoadhimisha miaka 10 tangu kuanzishwa kwake mwezi Machi mwaka 2012.

# Samia amulika nidhamu ya woga

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan ametaja sababu za kufanya mabadiliko madogo ndani ya Baraza la Mawaziri huku akibainisha kuwapo nidhamu ya woga serikalini.

Akizungumza jana Ikulu Chamwino, Dodoma mara baada ya kuwaapisha wateule wake aliowateua hivi karibuni, Rais Samia alisema mabadiliko yametokana na kuangalia nani anafaa kukaa wapi ili wakuze uchumi wa nchi kwa pamoja.

"Mabadiliko yaliyofanyika kwa upande wa mawaziri ni marekebisho tu ya kuangalia nani anafaa kukaa wapi kwa sababu wote bado tunasomana," Rais Samia alibainisha.

Walioguswa katika mabadiliko madogo ndani ya Baraza la Mawaziri yaliyofanyika hivi karibuni ni George Simbachawene, aliyekuwa Waziri wa Katiba na Sheria, amehamishiwa Ofisi ya Waziri Mkuu (Bunge, Sera na Uratibu) na Dk. Damas Ndumbaro, aliyekuwa Waziri wa Maliasili na Utalii amepelekwa Wizara ya Katiba na Sheria.

Mwingine ni Balozi Pindi Chana, aliyekuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Bunge, Sera na Uratibu), amekuwa Waziri wa Maliasili na Utalii.

Akiwachambua mawaziri hao, Rais Samia alisema Simbachawene ni mzoefu bungeni, akitamka: "Umekaa sana bungeni, ni bingwa wa sheria, nikaona uende kwa Waziri Mkuu, ukamsaidie kazi za Bunge na Sera kwa sababu una uzoefu mkubwa.

"Lakini kwa urefu wako na 'vimvi' vimeanza, unaweza kumsaidia vizuri Waziri Mkuu kuratibu wenzio, sauti yako ukisema wenzio watakutizama hivi (kwa juu) kuliko ambavyo wangemtizama Pindi, nimehisi uende pale utafanya vizuri zaidi."

Akimzungumzia Dk. Ndumbalo Rais Samia alisema, "Na miwani yako unaonekana jaji, mwanasheria kuliko kule kwenye Sekta ya Utalii, ndiyo maana nikaona uende kwenye hiyo wizara ukasimamie sheria zetu, marekebisho panapolega ukaze nati."

Kuhusu Balozi Chana, Rais Samia alisema ni mwanasheria na ameshapita kwenye diplomasia na uongozi wa maliasili na utalii anahusika na hilo, ndiyo maana ameona huko atakaa vizuri kuliko alikomweka awali.

"Kwa hiyo haya ni mabadiliko ya kawaida ya nani anafaa kukaa wapi, lakini kwa kuchekacheka nako huko (Chana) nadhani pia ni sifa mojawapo kwenye Sekta ya Utalii.

**BARAZA LA MAADILI**

Kuhusu Baraza la Maadili, Rais Samia alisema amekuwa akijiuliza suala la Tume ya Maadili na Baraza la Maadili.

"Nilikuwa sijawahi kulisikia Baraza la Maadili, nalisoma lakini nilikuwa sijawahi kupokea ripoti ya Baraza la Maadili, nikaambiwa wapo, waliteuliwa mwaka 2019, wengine baadaye lakini hawajaapa.

"Nikasema waite, Kwa hiyo baraza halijaanza kazi, sasa tume inafanyaje kazi kama baraza halipo? Kwa hiyo 2019 mpaka sasa mnamaliza kipindi chenu cha miaka mitatu kama wote mliteuliwa sawa.

"Pengine tunafanya mchanganyiko, pengine kesi za maadili zinakwenda TAKUKURU (Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa) au zinakwenda kwenye tume za utumishi lakini kumbe baraza lipo halifanyi kazi, nimeona muape na muanze kazi mara moja," aliagiza.

**NIDHAMU YA WOGA**

Rais alisema hali ya utumishi wa umma siyo nzuri na kwamba wanasifiwa marekebisho yaliyofanyika 2015 kidogo yamekuza heshima ndani yake.

"Heshima iliyokuzwa ni heshima ya woga kwa sababu kulikuwa na 'Simba wa Yuda' ambaye ulikuwa ukimgusa sharubu anakurarua lakini hata hivyo hatukukua kivile.

"Heshima inayotakiwa iwe ya moyoni, kila mmoja awe nayo itikadi moyoni mwake kwamba 'mimi ni mtumishi wa serikali, majukumu yangu ni haya, mstari wangu ni huu, itakiwi kuvuka huku', kila mmoja aheshimu mstari wa mwenzake.

"Ndicho tunakosa serikalini, kila siku unasikia waziri huyu kaparurana na katibu, Katibu Mkuu kaparurana na naibu wake, naibu sijui hamheshimu waziri wake, nani sijui hamheshimu nani, ninadhani kuna kitu tunakosa mahali," alionya.

Alisema wanakwenda kukiimarisha Chuo cha Utumishi na Chuo cha Uongozi ili vitoe mafunzo kwa Watanzania.

"Urais ni taasisi, siyo mtu! Kwa hiyo, wote tukifanya kazi kwa pamoja tutakwenda vizuri zaidi... niwaombe sana mkanisaidie, mkafanye kazi.

"Huko nyuma nilisema sitofoka, sitofokea mtu, nitafanya kazi kwa kalamu, nadhani ndicho ninachokifanya. Nitawakumbusha lakini sitofoka kwa sababu hata ukinitizama sijaumbwa kufokafoka, na mimi ni mama, ni mlezi, nitajaribu kuwalea lakini ulezi utakaponishinda nitachukua hatua kali," alionya.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa aliwaeleza wateule hao kuwa ofisi yake ipo wazi wakati wote, hivyo washirikiane kukamilisha majukumu waliyopewa ili yatoe matokeo ambayo wakati wote Rais amekuwa akiyasisitiza.

Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, aliwaahidi kuwa Bunge lipo tayari kushirikiana nao katika sekta ambazo wanakwenda kumsaidia Rais kuziongoza.

# LATRA CCC wakunwa mwitikio tiketi mtandao

**Na Costantino Mihambo,** TUDARCO

KAIMU Katibu Mtendaji wa Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Usafiri Ardhini (LATRA CCC), amewaomba abiria wa mabasi kutoa ushirikiano mkubwa katika majaribio ya mfumo wa tiketi mtandao ulioanza Aprili Mosi mwaka huu.

Leo Ngowi alitoa rai hiyo jana alipozungumza na waandishi wa habari na baadhi ya abiria kwenye Kituo cha Mabasi Magufuli kilichoko Mbezi Luis mkoani Dar es Salaam.

Alisema kuwa baada ya kufika kituoni huko ikiwa ni siku za mwanzo za utekelezaji wa majaribio ya ukataji tiketi kwa njia ya mtandao, baraza limeshuhudia mwitikio mkubwa kwa kuwa mabasi mengi yameanza utekelezaji wa agizo hilo na abiria wengi wamehamasika.

Ngowi alisema matumizi ya mfumo huo ni rahisi na abiria wameanza kuwa na uelewa juu ya faida za ukataji tiketi kwa njia ya mtandao.

"Mfumo huu unamwezesha abiria hata kama hana simu janja, ana uwezo kwenda kwa wakala wa basi na kusaidiwa kukata tiketi mtandao, lakini pia mtu yeyote mwenye simu janja anaweza kumkatia tiketi mwenzie. Mfumo huu ni rafiki kwa mtumiaji," alisema Ngowi.

Akitoa maelekezo jinsi ya kutumia mfumo huo, alisema kuwa mtumiaji anatakiwa kwenda kwenye 'play store' ya simu yake kisha kupakua mfumo wa tiketi mtandao na baada ya kupakua anapata taarifa ya mabasi yote kwenye kiganja chake na atachagua basi analotaka kusafiri nalo.

Alisema kuwa baada ya hapo ataanza kuingiza taarifa zake kwenye mfumo kama utakavyomwelekeza.

"Taarifa hizo ni kama vile tarehe ya kusafiri, kituo cha kuanzia safari, kituo cha kumalizia safari, namba ya simu, siti ya gari, kisha baada ya hapo atapokea taarifa kwamba ombi lake limekubaliwa.

"Baada ya kukubaliwa itakuja hatua ya kufanya malipo na baada ya kufanya malipo, ujumbe utatumwa kwenye simu yake ya kiganjani," alifafanua.

Kaimu Katibu Mtendaji huyo alisema baraza limejipanga kikamilifu katika utoaji elimu juu faida ya matumizi ya mfumo wa tiketi mtandao kwa abiria kwa njia mbalimbali kama vile kuwafikia kwenye vituo vya mabasi, kwa kutumia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi), Gabriel Migire, alitangaza kuanza rasmi kwa mfumo wa majaribio ukataji tiketi kwa njia ya mtandao Aprili Mosi mwaka huu na mfumo huo wa majaribio utakwenda kwa muda wa miezi mitatu na kwamba Julai Mosi mwaka huu, ukataji tiketi kwa njia ya mtandao utakuwa lazima.

# Serikali kuwekeza zaidi kwenye sekta ya uzalishaji

**Na Benny Mwaipaja,** DODOMA

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, ameliambia Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) kwamba Serikali imejipanga kikamilifu kuhakikisha kuwa sekta muhimu za uzalishaji zinaongezewa fedha ili kuongeza tija katika sekta hizo.

Dk. Nchemba alieleza kuhusu kusudio hilo alipokutana na kufanya mazungumzo na ujumbe wa Shirika hilo ukiongozwa na Mwakilishi wake Mkazi, Christine Musisi, jijini Dodoma.

"Katika Bajeti ya mwaka 2022/2023, na zijazo, tutawekeza fedha nyingi kwenye maeneo ya uzalishaji ikiwamo kilimo kwa kuongeza huduma za umwagiliaji na uzalishaji wa mbegu bora, uhifadhi wa mazao, mifugo bora, uvuvi na kuboresha mazingira ya biashara kwa wamachinga," alieleza Dk. Nchemba.

Alisema sekta hizo ni kipaumbele cha Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan, na inakwenda sambamba na utekelezaji wa Dira ya Taifa ya mwaka 2025 na Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

Aliipongeza UNDP kwa kuchangia maendeleo ya nchi katika nyanja mbalimbali za kiuchumi na kijamii, na kuliomba Shirika hilo kuendelea kuunga mkono juhudi za Serikali za kuwaletea wananchi maendeleo.

Naye Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Amina Khamis Shaaban, alisema Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano unakadiriwa kugharimu Shilingi trilioni 114.8 ambapo kati ya fedha hizo, Shilingi trilioni 40.6 zinatakiwa zitoke Sekta Binafsi na kuliomba UNDP kusaidia upatikanaji wa fedha hizo kwa kushirikiana na washirika wake mbalimbali.

Kwa upande wake Mwakilishi wa UNDP, Musisi, aliihakikishia Tanzania kwamba Shirika lake litaendelea kushirikiana nayo kuchangia maendeleo ya kiuchumi na kijamii kupitia miradi mbalimbali iliyowekeza fedha nchini, ikiwamo kilimo, uchumi wa bluu na kuboresha sekta nyingine za uzalishaji.

Aliahidi kuwa Shirika lake litaendelea kutoa fedha kwenye maeneo ya uzalishaji na uwekezaji kupitia Wizara ya Fedha na Mipango, lakini pia kuwashawishi wadau wengine kote duniani kuwekeza fedha katika maeneo mbalimbali ya uwekezaji yatakayochangia kuondoa umasikini na kutanzua vikwazo vyote kwa uzalishaji mali kupitia sekta binafsi na wajasiriamali.



Mufti wa Tanzania, Sheikh Abubakar Zubeir Bin Ally (wa pili kushoto), akipongezwa na Mkuu wa Kitengo cha CRDB Al-Barakah Banking, Rashid Rashid, wakati wa hafla ya kuukaribisha mwezi mtukufu wa Ramadhan pamoja na kumpongeza kwa kutunukiwa shahada ya udaktari wa heshima (PhD) na Chuo Kikuu cha Gambia, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## MIAKA 100 YA NYERERE

# Zitto, wadau wajadili Azimio la Arusha

**Na Jenifer Gilla**

KIONGOZI wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, na wadau wa siasa wamejadili kuhusu miaka 100 tangu kuzaliwa kwa Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, wakiutazama utekelezaji wa Azimio la Arusha.

Katika mjadala huo uliofanyika jijini Dar es Salaam jana, Zitto alisema kwa mazingira ya sasa nchini, ni muhimu kuhakikisha wenye mitaji hawawanyonyi wafanyakazi katika suala la ulipaji kodi.

"Utafiti nilioufanya mwaka 2017 kuhusu mwenendo wa ulipaji kodi kati ya wafanyakazi na wenye mitaji, niligundua kuwa wafanyakazi wanalipa kodi mara mbili zaidi ya wenye mitaji kwa sababu ni rahisi kukusanya kodi ya wafanyakazi kupitia PAYE tofauti na wafanyabiashara," alisema.

Zitto aliongeza kuwa wanapozungumzia msingi wa Azimio la Arusha, wazingatie mazingira yalipo sasa ya kiuchumi kwa kuwa wakati linatangazwa kwa mara ya kwanza, hali ya uchumi ilikuwa tofauti na sasa, kwa maana ya sekta ya uzalishaji na maeneo ya utumiaji.

"Wakati ule sekta kuu ya uzalishaji ilikuwa kilimo, na sehemu kubwa ya mapato ya kigeni ilikuwa ni kilimo, tofauti na sasa hivi ambapo tunavyo vingi ikiwamo dhahabu, utalii," alisema.

Zitto aliongeza kuwa ingawa lengo la Azimio la Arusha lilikuwa ni kuweka usawa katika umiliki wa mali lakini kiuhalisia lilikuwa ni ubepari wa kidola.

Alifafanua kuwa mara baada ya Azimio la Arusha, serikali ilitaifisha njia kuu za uchumi kutoka kwa watu binafsi na kuzimiliki kwa niaba ya wananchi ikiwamo viwanda, benki, njia za usafirishaji, jambo ambalo kwake anaona ulikuwa ni ubepari wa kidola.

Sabatho Nyamsenda, mwalimu wa sayansi ya siasa katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), alisema msukumo mkubwa wa kulitaka Azimio la Arusha ulitoka kwa wananchi baada ya kuona kuwa uhuru unawanufaisha wachache wenye nacho na kuwanyonya wengi wasionacho.

Alisema kuwa moja msingi ya Azimio la Arusha ni kubomoa ubepari na kujenga ujamaa kwa kuziweka njia kuu za uzalishaji mali mikononi mwa umma kwa njia mbili - dola na vyama vya ushirika na kuondoa msingi wa ukoloni mamboleo.

"Maana yake ni kwamba unaondoa ule unyonyaji wa watu wachache wanaofaidika na sehemu kubwa ya jasho na rasilimali zilizopo nchini na sasa zinaenda kuleta faida kwa walio wengi," alisema.

Mshiriki wa mdahalo huo kutoka Mtwara, Said Manoro, alisema alikuwapo kipindi azimio hilo linapitishwa, akisisitiza kuwa nchi haiwezi kutoka nje ya azimio hilo kwa kuwa ndiyo msingi wake.

"Mimi natembea na Azimio la Arusha, kutoka nje ya msingi ya Azimio la Arusha ni kupoteza muda, Azimio la Arusha ndiyo Tanzania na ndiyo Watanzania, ndiyo serikali ya wananchi," alisema.

Mshiriki wa mdahalo, Christina Mfinanga, alisema wanapozungumzia Azimio la Arusha, wawaangalie wananchi wa hali ya chini ambao misingi ya azimio hilo iliwekwa kwa maana ya usawa katika umiliki wa uchumi.

RIPOTI MAALUM

# Risasi iliyomuua mwanakijiji mgodini inavyozua mtafaruku

## ▪Vitendawili vyagubika mkasa mzima
## ▪Tegemeo la wazazi, mke na kichanga

**Na Mwandishi Wetu,** KISHAPU

TULIMKUTA akiwa ameanguka chini, amepigwa risasi paja la kulia, ikatokea upande wa pili. Hata 'kulwa na doto' (sehemu za faragha) walikuwa wamebomolewa vibaya," Yunge Sheka, mkazi wa Kitongoji cha Mwamala, Kijiji cha Igumangobo wilayani Kishapu, anakumbuka mkasa uliojaa simanzi na chanzo cha kifo cha mtoto wake wa kwanza.

Yunge (48), akiwa ameketi kwenye gogo nje ya nyumba yake, mwili wake akiutanda kwa khanga, anaendelea kusimulia kuwa ilikuwa Machi 10, mwaka huu kijiji hicho kilipotawaliwa na simanzi pale kijana wao, Cosmas Hamis (23), alipofariki dunia kwa kupigwa risasi jirani na mgodi wa almasi wa El Hilali, mahali ambako siyo mbali na alikokuwa anaishi.

Hapo ni umbali wa Km 23.6 kaskazini mashariki mwa Mji wa Shinyanga na safari yake kwa gari kutoka mjini Shinyanga inachukua takriban nusu saa ukifuata barabara ya lami ya Shinyanga-Mwanza kisha unachepuka kulia kuifuata barabara ya vumbi kupitia Utemini, kijiji maarufu kwa watafutaji wa almasi nchini.

Yunge anasema ni mkasa ulioibua taharuki na mvurugano, akisimulia kwamba siku hiyo mwanawe Cosmas waliyekuwa wanaishi naye, aliwafuata shambani saa tatu asubuhi, akiwaaga anakwenda kutafuta riziki.

Mama huyo anaendelea kuwasilisha kilichojiri kwamba, wakiwa wamesharejea nyumbani, wakapata taarifa mtoto wao amepigwa risasi na amedhurika vibaya katika eneo jirani na mgodi huo.

Yunge anasema ni taarifa zilizowafanya wachukue uamuzi wa haraka kuelekea eneo la tukio, ambako siyo mbali na wakaushuhudia ukweli huo.

Anasema kuwa mara moja, baba wa marehemu kwa kushirikiana na wanaume wenzake, walichukua gari kumwahisha kwenda Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Shinyanga kwa ajili ya matibabu.

Mama huyo anayezungumza kwa sauti ya chini, inafika hatua simanzi inamtawala, anasita kuendelea na ufafanuzi wake, akihamia kwenye kilio.

Wakati Nipashe ikiendelea kudadisi, baba wa marehemu, Hamis Kushilimwa (50), analazimika kuendeleza mazungumzo hayo, akifafanua kwamba wakiwa njiani kuelekea hospitalini, mwanawe akawa anaendelea kutokwa na damu nyingi na hatimaye umauti ukamkuta umbali si mrefu na wote wakaridhiana kuurejesha mwili eneo la tukio.

Anasimulia kwamba baada ya kurudi eneo la tukio, waliushusha mwili na kupiga mbiu ya kimila, iliyokusanya umma wa kijijini ukiongozwa na askari wa sungusungu waliozonga eneo hilo, wengi wakiwa na hisia za 'hatukubali'.



Baba mzazi wa marehemu Cosmas, Hamis Kushilimwa (wa pili kulia), akifanya mahojiano na Ofisa Mipango Mwandamizi wa LHRC, Wakili Joyce Komanya, kijijini Igumangobo wilayani Kishapu hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



BURIAL PERMIT ........ NO. 028/3/2021
NAME: COSMAS HAMIS
AGE: 23 SEX: M NATIONALITY TRIBE: Sukuma
(If unknown, state child, adult or aged person).
DATE OF DEATH: 10/03/2022 RELIGION: ........ DISEASE (1): Hypovolemic Shock 2° Penetrative Wound
Certified / Notified by Matinde J. D...
HEALTH OFFICE SRRH
MEDICAL OFFICER IN CHARGE SHINYANGA 11 MAR 2022
Medical Officer of Health
Section 44 of the TOWNSHIP Rules, 1923 – (4) No person shall burry, cremate or otherwise dispose of the corpse of any person who has died within the Township without a permit signed by the Medical Officer of Health or if there be no Medical Officer of Health by a Government Medical Officer or in default by and administrative Officer.

Kibali cha kuzika mwili wa Cosmas Hamis kilichotolewa na Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Shinyanga.

> **"Tulimkuta akiwa ameanguka chini, amepigwa risasi paja la kulia, ikatokea upande wa pili. Hata 'kulwa na doto' walikuwa wamebomolewa vibaya"**

Kwa mujibu wa mzazi huyo, ni hali ya mshikemshike iliyotawala mahali hapo na kijiji kizima, ujumbe ukifika ng'ambo kutoka waliko mgodini na ilipotimu saa saba usiku, polisi waliwasili na gari lao wakiwa na diwani na mwenyekiti wa kijiji, wakaomba wananchi wawe watulivu, hata wakapewa mwili kwa ajili ya uchunguzi hospitalini.

Kushilimwa ananukuu mrejesho wa kwanza waliopewa hospitalini kwamba uchunguzi ulifanywa Machi 11 na kilichogundulika mwanawe alipigwa risasi katika namna aliyoieleza mama yake na siku iliyofuata Machi 12 walikabidhiwa mwili.

Hapo ndipo baba huyo anasema ukaibuka utata wenye sura mbili. Mosi; hata kabla ya kuupokea mwili huo, hawakuwa tayari kuuchukua kwani kiuchumi walikuwa hoi, hawana pesa za kuusafirisha kutokana na hali yao duni, huku mtegemezi wao ndiye aliyetangulia mbele ya haki.

Pia ufafanuzi wa kisheria walipewa kutoka kwa Ofisi ya Upelelezi ya Polisi Mkoa wa Shinyanga, ulibainisha Cosmas aliuawa na polisi waliotumia bunduki aina ya 'Sub Machine Gun', maarufu SMG.

Kwa mujibu wa baba wa Cosmas, ufafanuzi huo ulimwekea utata kwenye uelewa wake kwani kwa hatua zote za awali na ilivyoeleweka hata kijijini kwake Igumangobo, kitendo hicho kilifanywa na askari wa mgodini.

Anasema kutokana na sintofahamu ya kipato, Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai Mkoa (RCO) ambaye hakumtaja jina, aliwakabidhi Sh. 100,000 kwa ajili ya kukodi gari la kuusafirisha mwili, tayari kwa maziko kijijini.

"Mwili ulipofikishwa hapa nyumbani, ulizikwa na umati mkubwa wa watu ukizingatia askari wa sungusungu nao walikusanyika hapa kutokana na kifo cha mwanangu kuwa cha uonevu," Kushilimwa anasema.

**MWENYEKITI WA KIJIJI**

Abeid Jilala, Mwenyekiti wa Kijiji cha Igumangobo kilichoko Kata ya Idukilo, ana ufafanuzi zaidi kuhusu tukio la mauaji ya kijana huyo na hatua zilizochukuliwa, akitamka:

"Cosmas alipigwa risasi akiwa karibu na eneo la machimbo ya almasi katika Kijiji cha Mwanholo, Kata ya Lohumbo. Tulimkuta damu inamwagika kama maji.

"Polisi walifika saa 7:14 usiku, kabla hawajafika eneo la tukio, wananchi waliambiwa wapungue, waende majumbani maana wengi wao walikuwa wamekasirishwa na mauaji hayo. Kilichofuata sisi viongozi tuliwaachia polisi wafanye uchunguzi ili serikali ichukue hatua stahiki.

"Licha ya tukio hilo, bado wananchi wanaendelea kwenda kuchimba. Mvua mwaka huu imegoma, tegemeo pekee la kipato kwa sasa hapa ni uchimbaji wa madini.

"Vijiji vinavyowika sana kwa kutoa mawe (almasi) ni Mwanholo na Nyenze. Wachimbaji wanatoka vijiji jirani na maeneo haya vya Ikudiko, Utemini, Buganika, Maganzo, Masagala, Wizunza, Buchambi na hata Kolandoto."

**KAULI YA MGODI**

Antony Rafael, Kaimu Meneja wa Mgodi wa El Hilali, katika mazungumzo na Nipashe, anakiri askari polisi waliokuwa wanalinda mgodi wao, walihusika katika mauaji ya kijana Cosmas.

"Kilichotokea ni kwamba waliingia hapa mgodini kwa kutuvamia, walikuwa wengi, zaidi ya 20. Wengi walikimbia baada ya polisi kufyatua risasi hewani, walibaki watatu wakawa wanapambana na polisi.

"Kuna mmoja wa askari aliyejeruhiwa, katika kujihami ndipo akampiga risasi huyo aliyefariki dunia (Cosmas). Ndicho kilichotokea, hakuna tukio lingine zaidi kwa sasa tangu lilipotokea hilo (la mauaji ya Cosmas)," Rafael anasema.

Nipashe inapohoji uhalali wa askari walinzi wa mgodi kuua watu kwa kuwapiga risasi, Rafael ana ufafanuzi, akitamka: "Hao ni wavamizi. Mtu amekuvamia, lazima ujihami. Sasa katika huko kujihami, ndicho hicho kilichotokea."

**HOSPITALINI SHINYANGA**

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Shinyanga, Dk. Luzila Boshi, katika ufafanuzi wake kwa Nipashe kuhusu kifo cha Cosmas, anakiri hospitali hiyo kuufanyia uchunguzi mwili wa kijana huyo.

"Ni kweli tuliupokea mwili wa Cosmas Machi 11, mwaka huu na wataalamu wetu hapa waliufanyia 'postmortem' (uchunguzi). Mwili uliletwa hapa hospitalini na polisi ili ufanyiwe uchunguzi, ulikabidhiwa kwa ndugu Machi 12, mwaka huu.

"Yule mtu (Cosmas) alikuwa anasadikiwa kupigwa risasi. Sisi tulifanya postmortem na matokeo ya postmortem tuliwakabidhi polisi.

Kwa mujibu wa taratibu za kisheria, wao (polisi) ndiyo wenye mamlaka ya kutangaza kilichobainika kwenye postmortem," anafafanua.

Kwa mujibu wa kibali cha kuzika mwili wa Cosmas kilichotolewa na Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Shinyanga Machi 11 mwaka huu, chanzo cha kifo cha kijana huyo kimetajwa kwa lugha ya kitabu kwamba ni 'Hypovolemic shock secondary to penetrative wound'.

Kwa tafsiri isiyo rasmi, ni hali ya dharura ambayo kunatokea upotevu wa damu nyingi au maji mwilini, hivyo kufanya moyo kushindwa kusukuma damu ya kutosha mwilini. Kibali kinaonyesha hali hiyo kwa Cosmas ili sababishwa na jeraha lililotokana na kitu chenye ncha kali.

●ITAENDELEA JUMAPILI IJAYO

# Mil. 471/- zakopesha wajasiliamali Halmashauri Wilaya Igunga

**Na Jumbe Ismailly,** IGUNGA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Igunga,mkoani Tabora imetoa mikopo yenye thamani ya shilingi 471,787,617.01 kwa vikundi vya wajasiriamali wa makundi ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu katika kipindi cha kuanzia Julai-Septemba 2021/2022 hadi Oktoba – 2021/2022.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri ya Wilaya ya Igunga, Godfrey Chezue, alibainisha taarifa hiyo wakati wa hafla ya utoaji mikopo kwa robo ya mwaka kuanzia Oktoba hadi Desemba, 2021/2022 yenye thamani ya jumla ya shilingi 88,204,678.01 kwa vikundi 14 vya wanawake,vijana na watu wenye ulemavu iliyofanyika Halmashauri ya Wilaya ya Igunga.

Aidha Chezue alifafanua kwamba fedha hizo zinazotolewa kwa lengo la kuwezesha wananchi kiuchumi zinatokana na asilimia kumi ya makusanyo yake inayotengwa kutokana na mapato yake ya ndani.

Aidha, alisema kwamba idara ya maendeleo ya jamii katika Halmashauri ya Wilaya ya Igunga imeendelea kuwawezesha wananchi kiuchumi kwa kutoa mikopo kwa makundi hayo ikiwa ni utekelezaji wa Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa,sura 290 na kanuni za utoaji na usimamizi wa mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ya mwaka 2019 kama ilivyofanyiwa marekebisho Februari mwaka 2021.

Chezue alibainisha kuwa katika mwaka wa fedha wa 2021/2022, Halmashauri ya Wilaya ya Igunga ilitekeleza miradi ya maendeleo kwa kutenga jumla ya shilingi 228,700,000/= kupitia asilimia kumi ya makusanyo ya mapato ya ndani inayotengwa na kupelekwa Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake,Vijana na Watu wenye Ulemavu.

Kwa mujibu wa Ofisa huyo, katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2021/2022 katika robo ya mwaka kuanzia Julai – Septemba 2021/2022,Halmashuri hiyo imekabidhi mikopo yenye thamani ya shilingi 113,980,600.

Alisema kwamba katika fedha hizo zilizotolewa katika robo ya Oktoba- Desemba 2021/2022 jumla ya vikundi 7 vya wanawake vilikabidhiwa shilingi 41,902,339, wakati vikundi sita vya vijana vilipokea shilingi 41,302,339 na kikundi kimoja cha watu wenye ulemavu kilikabidhiwa shilingi milioni 5.

Wakizungumza baada ya kupokea mikopo hiyo baadhi ya wajasiriamali hao waliishukuru serikali.

Magreth Benjamin, Wakulu Juma, Hamisi Kafumu na Kimali Busagara kwa nyakati tofauti walisema wanaishukuru serikali kwa kutoa mikopo hiyo isiyokuwa na riba kwani itawasaidia kufanya biashara zao bila misukosuko yoyote na kwamba mikopo hiyo imesaidia pia kupunguza ukosefu wa ajira kwa vijana kwani wao wanaenda kujiajiri kwa kupitia biashara zao.

# Maaskofu wastaafu KKKT wapewa somo

**Na Thobias Mwanakatwe,** MOSHI

MAASKOFU wastaafu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) nchini wametakiwa kutokufukua mbegu walizozipanda wakati wa uongozi wao katika kanisa ili kuepusha migogoro ambayo inalichafua kanisa ndani na nje.

Aidha, wameombwa kuendelea kulibeba kanisa la Mungu kwa utulivu na kwa unyenyekevu ili kuepukana na mpasuko na migogoro inayoepukika.

Wito huo ulitolewa na Mchungaji Delton Boaz Mbuya, ambaye ni msaidizi wa Askofu wa KKKT Dayosisi ya Ziwa Tanganyika, Ambene Mwaipopo katika mahojiano maalumu na gazeti hili mjini Moshi kufuatia mgogoro unaoendelea katika Dayosisi ya Konde mkoani Mbeya.

Alisema kwa hali ilivyo kinachojionyesha ni kama baadhi ya watumishi wa kanisa hilo wamekosa hofu ya Mungu kwa kutoheshimu mamlaka za juu za kanisa hilo ambazo wamezi-weka wao wenyewe.

"Natoa wito kwa Maaskofu wastaafu kutokufukua mbegu walizozipanda, tuwaombe waendelee kulibeba kanisa la Mungu kwa utulivu na kwa unyenyekevu, kwani kuendelea kufanya hivyo kanisa litakuwa na mpasuko mkubwa huko mbeleni utakaokuwa umetokana na ukosefu wa busara za hao wastaafu," alisisitiza Askofu Mbuya.

Askofu Mbuya alisema wako baadhi ya maaskofu wastaafu ambao walitegemewa wangesaidia kutokuruhusu mpasuko, lakini kwa sasa kanisa linakwenda kwenye mpasuko kutokana na wao kufukua mbegu walizozipanda wakiwa bado watumishi. "Tunahitaji kuheshimu mamlaka ambazo tumeziweka na kuzisikiliza tuache malumbano ambayo yanakwenda kulivuruga na kulichafua kanisa," alisema.

"Mgogoro unaoendelea katika Dayosisi ya Konde ni matokeo ya baadhi ya watumishi na viongozi kutotii mamlaka walizoziweka wenyewe kwani Kanisa la KKKT lina utaratibu wake, hata migogoro ya siku za hivi karibuni inasababishwa na hali hiyo," alisema.



Sadick Ngwiso, Mkazi wa Kijiji cha Luhunga, kitongoji cha Igoda, wilaya ya Mufindi, mkoani Iringa, akigema ulanzi kijijini hapo jana. Ulanzi ni pombe ya asili inayopendwa sana na wenyeji wa mkoa huo. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Wizi wa bodaboda ulivyompeleka jela

**Na Said Hamdani,** LINDI

MAHAKAMA ya Wilaya ya Lindi, imemhukumu mkazi wa Kata ya Mtanda, Hassani Ally Lihami (33), kutumikia kifungo cha miaka minne gerezani, baada ya kupatikana na hatia ya wizi wa pikipiki yenye thamani ya Sh. 2,250,000/.

Hukumu hiyo ilitolewa na Hakimu Mkazi Mfawidhi Maria Betraine, baada ya kujiridhisha na ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka.

Baada ya Mahakama kumuona ana hatia, mshtakiwa aliulizwa iwapo analo neno la kuishawishi ili isimpe adhabu kali, aliomba imuonee huruma kwa madai ni kosa lake la kwanza.

Pia,alidai anayo familia akiwamo mke na watoto wanne wanaomtegemea, hivyo kama atapewa adhabu kubwa kutaifanya ikose huduma zake.

Baada ya utetezi huo, Hakimu Batrane alimuuliza Mwanasheria wa Serikali, Godfey Mramba, iwapo anazo kumbukumbu za makosa ya zamani kwa mshtakiwa, na kujibu hana, aliiomba mahakama kumpa adhabu kali ili iwe fundisho kwake na wengine wenye tabia ya wizi.

"Naiomba Mahakama yako tukufu impe mshtakiwa adhabu kali kukomesha hii tabia ndani ya Mkoa wetu wa Lindi," alisema Mramba.

Hakimu Batraine akitoa hukumu katika kesi hiyo ya jinai namba 644/2021,kupitia vifungu 258 (1) na 265 cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu sura ya 16 rejeo 2019, alisema amesikia ushahidi wa pande zote, hivyo anamhukumu kutumikia kifungo cha miaka minne gerezani na kulipa fidia ya Sh. 2,250,000.

Awali ilidaiwa na Mramba kuwa mshitakiwa alifanya wizi huo Septemba 16/2021 eneo la Kata ya Mkumbi, kwa kuiba pikipiki aina ya Sanlg namba za usajili MC 909 CMB yenye thamani ya Sh. 2,250,000/, mali ya Isumaili Issa Omari.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# EAC iihakikishie usalama Congo

**WIKI** iliyopita Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) ilipatiwa uanachama rasmi ndani ya Jumuiya ya Afrika Mshariki (EAC), hivyo jumuiya hiyo iliyoanzishwa mwaka 1967 kufikisha wanachama saba.

Hatua ya kuipatia uanachama DRC imepongezwa sana kwamba itanufaika kiuchumi kutokana na mipaka yake kufunguka na fursa nyingine ambazo itazipata kutokana na kujiunga na nchi za EAC ambazo nyingi inapakana nazo.

Kimsingi mengi yamezungumzwa na kuhusiana na kupokelewa kwa taifa hilo lenye ukubwa kuliko yote kwa eneo barani Afrika katika EAC na manufaa yake na wanachama wake.

Wanazuoni wabobezi katika masuala ya mtangamano (integration) wanaeleza sababu mbalimbali zinazozifanya nchi kuungana ama kushirikiana kikanda kwamba msukumo mkubwa ni kupata; kwa maneno mengine ni kunufaika katika mambo ambayo nchi husika inaona hayaiendei sawa.

Sababu hizo ni kunufaika kiuchumi hata kama mataifa hayo yana udugu wa kihistoria au ujirani wa mipaka. Hata hivyo, kuna sababu nyingine ya tishio la usalama ambayo huzilazimisha baadhi ya nchi kujiunga katika ushirikiano ili kujihakikishia usalama.

Sababu zote hizi zinaigusa DRC hususan ya tishio la usalama. Ikumbukwe kwamba taifa hilo tangu baada ya kupata Uhuru wake kutoka Ubelgiji mwaka 1960 halijawahi kupata amani ya kudumu hadi leo hii. Haikuchukua muda Waziri wake Mkuu wa kwanza, Patrice Lumumba akauawa ndani ya mwaka mmoja kisha kutumbukia katika utawala wa kidikteta wa Mobutu Sesseseko ambao ulisababisha madhila makubwa kwa Wacongo hadi mapinduzi yaliyomwondoa madarakani kwa njia ya vita.

Hata mrithi wake Laurent Kabila aliyeingia madarakani 1998, utawala wake ulighubikwa na machafuko yaliyotokana na mapigano kati ya makundi mengi ya wapiganaji na jeshi la Serikali hadi kiongozi huyo alipouawa kwa risasi jijini Kinshasa mwaka 2001. Utawala wa mwanaye, Joseph Kabila nao haukuifanya DRC kupata amani kutokana na kusumbuliwa na mashambulizi ya makundi yenye silaha dhidi ya raia na kusababisha mauaji ya watu wasio na hatia na kuharibu mali hususan katika maeneo ya mashariki mwa taifa hilo lenye utajiri mkubwa wa rasilimali.

Hadi sasa katika utawala wa Felix Tshekedi, maeneo ya mashariki yanaendelea kukosa usalama kutokana na kuibuka upya matukio ya mauaji yanayofanywa na makundi hayo yanayoibuka kila uchao yakiwamo M-23 na EDF.

Tunaliona suala la usalama DRC kuwa ni la msingi na linapaswa kuchukuliwa kwa uzito mkubwa na wakuu wa EAC, kwa kuhakikisha nchi hiyo inapata usalama na amani ya kudumu ikiwa ni mwanachama mwenzao.

Hatua hiyo ndiyo itakayolifanya taifa hilo lishiriki ipasavyo katika utekelezaji wa shughuli zote za jumuiya, tofauti na kuwa mwanachama ambaye watu wake wanataabika kwa kukosa amani na utulivu. Hilo likifanyika linaweza kupunguza ukubwa wa tishio la usalama kwa nchi ambalo lilisababisha nchi hiyo iwe na idadi ya vikosi vya walinzi wa amani wa Umoja wa Mataifa (UN) nchini humo (MONUSCO) kufikia 18,000 mwaka 2017.

Kumekuwapo taarifa zakuzihusisha baadhi ya nchi, zikiwamo wanachama wa EAC kufadhili shughuli za makundi kadhaa ya waasi nchini humo, hivyo kuzorotesha mahusiano ya kidiplomasia. Iwapo nchi wanachama wa EAC zimedhamiria kwa dhati kushirikiana na kufikia malengo tarajiwa, tunazishauri ziweke mpango mkakati wa kuliangalia kwa jicho la pekee suala la usalama wa DRC. Hilo tunaamini kwamba litawezekana kama viongozi wakuu katika nchi wanachama watajenga uwazi na kuaminiana, ikiwamo kulijadili kwa uwazi kisha kufungua ukurasa mpya.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Mifumo ya TEHAMA imulikwe ili kutunza siri, kuepuka ubadhirifu

Na Sanula Athanas

**DESEMBA** 4, 2021, Rais Samia Suluhu Hassan alivunja Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Bandari (TPA) kutokana na ubadhirifu ulioubaini kuisababishia hasara serikali, akiweka wazi kuwa upotevu wa mapato unachangiwa na mifumo kutokuwa madhubuti.

Siku moja baada ya uamuzi huo wa Rais, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), Naghenjwa Kaboyoka, alipongeza hatua hiyo ya Mkuu wa Nchi, akisema kwamba kwa takriban miaka mitano kamati yake imekuwa ikiiagiza bodi hiyo kuhakikisha mifumo ya Bandari inafanya kazi kwa ufanisi na inasomana lakini utekelezaji wake haujafanyika kwa ufanisi.

Kimsingi, dosari katika mifumo zimechambuliwa kwa kina Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwenye ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka 2019/20.

Mnamo Machi 28, 2021, akiwa na siku tisa pekee tangu kuapishwa kushika wadhifa wa sasa, moja ya hatua zake muhimu za awali, Rais Samia alipokea Ripoti ya CAG kwa mwaka 2019/20.

Ndani ya mlolongo mrefu wa wasilisho lake, CAG, Charles Kichere, alichambua kasoro nyingi zilizoko katika ya mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) na utendaji wake serikalini.

Hata Machi 30, mwaka huu, Rais Samia alipopokea ripoti ya CAG kwa mwaka 2020/21, dosari katika mifumo ya TEHAMA zimetajwa tena na CAG kuwa sehemu ya upotevu wa mapato ya nchi.

Kwa kurejea historia ya nchi, mchakato wa kuwa na sera ya TEHAMA serikalini ulianza rasmi mwaka 2003, ikiwa ni kuendana na mageuzi yanayochukua kasi duniani katika eneo hilo.

Baada ya sera hiyo kudumu kwa zaidi ya muongo mmoja, mnamo Mei 16, 2016, serikali ilizindua sera hiyo iliyofanyiwa mapitio, na miezi sita baadaye, yaani Novemba 2016, ukiwa ni mwanzo wa serikali ya awamu ya tano, mwongozo maalumu wa matumizi yake ukazinduliwa.

Kwa mujibu wa Tovuti Kuu ya Serikali, miongoni mwa maudhui muhimu yaliyoshuhudiwa katika zama hizo za uzinduzi miaka mitano iliyopita, yalijumuisha mtazamo wa kuelekea kwenye manufaa katika kipindi hicho cha uzinduzi yakiwa na ufafanuzi:

Mosi ni manufaa ya mtandao unaoihakikishia serikali inakuwa kama taasisi moja kwa kuunganishwa na TEHAMA, huku usalama na faragha za taarifa za serikali na watumiaji ukiimarishwa.

Pili; kuwapo lengo kuu lenye mtazamo wa kurahisisha utendaji kazi wa serikali na kuboresha kwa kiasi kikubwa utoaji wa huduma kwa wananchi.

Tatu; kubeba mtazamo mahususi wa kupunguza gharama kubwa ya kuwapo mifumo ya TEHAMA serikalini, matumizi shirikishi na inayotumika kirahisi kwa walengwa wa huduma husika.

Pamoja na kuwapo sura hiyo ya manufaa wakati wa kuzindua mwongozo, tayari kulikuwa na angalizo la kasoro inayopaswa kurekebishwa inayonukuliwa kwa ujumbe ufuatao utokanao na angalizo la uzoefu wa matumizi ya TEHAMA serikalini.

Ushauri wa kiserikali uliotolewa kuweka sawa dosari hizo, ulitaka kujengwa uelewa wa viwango stahiki vya TEHAMA vinavyohitajika serikalini kwa sekta binafsi na umma.

Mbali na CAG kukiri kasi ya kutumika TEHAMA serikalini, bado ana angalizo maalumu kupitia ripoti ya ukaguzi wake ya mwaka 2019/20, akiwa na orodha ya udhaifu katika maeneo ya utekelezaji.

CAG Kichere anasema TEHAMA duni imeipotezea bajeti wajibu na haki yake kuwa nyenzo ya udhibiti wa shughuli za fedha serikalini, huku akitoa mfano hai wa kuwapo taasisi sita za kiserikali zilizotumia ziada ya jumla ya Sh. bilioni 24.41 nje ya kiwango kilichoidhinishwa katika mwaka wa ukaguzi (2019/20).

Vilevile, ananyoshea kidole athari za kuwapo mifumo miwili au zaidi inayofanya kazi zinazofanana kwamba ni hatua inayoiongezea serikali gharama zisizo za lazima katika uendeshaji na matengenezo, huku akiwa na ufafanuzi zaidi kwamba:

Kwa kutambua umuhimu wa hoja hizi, kuna haja serikali kuzifanyia kazi ili kutunza na taarifa za siri za nchi na kudhibiti ubadhirifu wa fedha za umma unaofanywa kwa kuichezea mifumo ya ukusanyaji wa mapato.

Dosari zilizoainishwa na Rais Samia kwenye Bandari, ni sehemu tu ya madhila mengi dhidi ya mapato ya serikali yanayofanywa na watendaji wasio waadilifu kupitia upungufu uliopo kwenye mifumo ya TEHAMA.

SAFU

## KWA MASLAHI YA TAIFA

# MWAKA MMOJA WA SAMIA:
# TARURA imefanya maajabu kutandika lami hadi vijijini, Ila...



Na Pascal Mayalla

MWEZI huu mzima, tunaendelea kushuhudia wizara, wakala, idara na taasisi mbalimbali za umma, zikitoa wasifu wa mafanikio ya mwaka mmoja wa serikali ya awamu ya 6 chini ya Jemedari Chifu Hangaya, Rais Mama yetu Samia Suluhu Hassan.

Taasisi nyingi zimefanya mengi, makubwa, mazuri, lakini mimi nimeguswa zaidi na kazi kubwa, nzuri ya kupendeza na ya kutukuka ya Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA), hawa sio tuu wamefanya makubwa, bali wamefanya maajabu!.

TARURA ni Wakala katika Wizara chini ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ambao ulianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Wakala za Serikali Sura Namba 245 na kutangazwa rasmi kwenye Gazeti la Serikali Na 211 la tarehe 12 Mei 2017. Wakala umechukua majukumu ya utekelezaji kuhusiana na ujenzi na matengenezo ya mtandao wa barabara za Vijijini na Mijini ambayo hapo awali yalikuwa yakitekelezwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Jukumu kubwa la Wakala ni usimamizi, ujenzi, na matengenezo ya mtandao wa barabara za vijijini na mijini ikijumuisha kuimarisha usalama wa barabara, kulinda hifadhi za barabara zisivamiwe na kudhibiti athari za mazingira na za kijamii.

Tangu kuzaliwa kwangu na miaka yangu zaidi ya 50, sikubahatika kuwahi kuona au kushuhudia, barabara za vijijini zikipigwa lami, lakini ndani ya huu mwaka mmoja wa Samia, nimeshuhudia kwa macho yangu, baadhi ya barabara za vijijini kabisa, 'deep interior', zimetandikwa lami!.

Haya ni maendeleo makubwa sana kuwahi kutokea Tanzania, tumezoea kuona barabara za vijijini ni za vumbi, au za changarawe, lakini hili la barabara za vijijini kuwekwa lami!, kongole kwa TARURA, TAMISEMI na Rais Mama Samia, sio tuu kwa ku double (kuongeza mara mbili), bajeti ya TARURA, bali ame triple kabisa (kuzidisha mara tatu).

Tanzania tuna mitandao miwili ya barabara, mtandao wa kwanza ni mtandao wa barabara za Tanroads, ambazo ni barabara kuu za mikoa, miji na wilaya, na mtandao wa barabara za TARURA, unaohusisha, barabara za vijijini na mijini.

Hii mitandao ya barabara inaitwa 'system', sasa ili 'system' zifanye kazi kwa ufanisi, lazima hizo 'systems', ziongee lugha moja. Wakati tunaanzisha ushuru wa pamoja kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, enzi hizo zikiwa tatu, Tanzania, Kenya na Uganda, tukajikuta mwanzoni tulikwama kwa sababu, mifumo ilikuwa haiongei lugha moja.

TRA ya Tanzania, tulikuwa tunatumia mfumo wa Ayscuda ++ (inatamkwa Ascuda plus plus), wakati Kenya na Uganda walikuwa wanatumia mfumo wa Simba. Baadaye mifumo ilioanishwa ikawa inazungumza lugha moja sasa mambo ya ushuru ni supa.

Vivyo hivyo, ili hii kazi nzuri ya TARURA kufungua barabara za vijijini kwa nyingine kupigwa lami, na kuleta manufaa makubwa kwa wananchi wetu wa vijini, ni iwapo mifumo hii miwili ya mitandao ya barabara nchini, yaani barabara za TANROADS na Barabara za TARURA, lazima ziongee lugha moja.

Mfano mzuri ni kule Kilolo , Iringa, TARURA imeipiga lami barabara ya kilomita 18, kutoka Kidabaga hadi Bomang'ombe. Lakini barabara inayotoka Kilolo hadi Kidabaga ni barabara ya vumbi, mvua zikinyesha, haipitiki!. Hivyo wakati wa masika, wakulima wa Bomangombe, watafaidi sana, kuleta mazao yao hadi Kidabaga lami ilipoishia, halafu kutoka Kidabaga kwenda Kilolo ni vumbi, na mvua ikiwa kubwa, inamaana safari yao itaishia Kidabaga, na mazao yao yataozea barabarani.

Wakati TARURA wanapanga kutandika lami barabara fulani kutokana na umuhimu wake kiuchumi, system ya TARURA isomeke TANROADS ili kama barabara hiyo inatakiwa kuwekwa lami na TARURA ni 'feeder road' kwa 'main road' ya TANROADS, kama TANROADS hawakuwa na mpango wa kuiweka lami hiyo barabara ya wilaya, basi waiingize kwenye mpango kazi wake ili kupata hiyo smooth accessibility, na sio kipande kizuri cha lami kijijini, halamu kipande kibovu cha vumbi, barabara ya Tanroad.

Tanroad waulizwe wataweka lini lami kipande hicho ili barabara yote ipitike wakati wote. Na ikitokea, TANROADS hawana kabisa mpango huo kwa kipande hicho, then TARURA wawasaidie TANROADS kukitia lami kipande hicho, kwa complementing each other, ila pia kwenye bajeti, TARURA wakisaidia TANROADS, bajeji ya TANROAD imegwe kupewa TARURA kuifidia kuisaidia TANROAD, na ikitokea kwa TANROAD barabara fulani ya kijijini TANROAD wamesaidia, bajeti ya TARURA inamegwa kufidia, ili TARURA wakifungua barabara ya kijiji fulani kwa kutandika lami, lazima TANROAD nao waifungue, hivi vipande vya lami, vumbi lami vumbi havinogi!.

Watanzania wenzangu, tuungane kuunga mkono kazi nzuri iliyofanywa na TARURA kwa kuipongeza bodi ya ushauri ya TARURA, uongozi, menejimenti na wafanyakazi wa Tarura, kwa kuzitunza barabara za vijijini na mijini, na bila kuacha kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan na serikali yake kwa kuiwezesha TARURA kuyafanya hayo baada ya kuiongeza bajeti ya TARURA mara tatu, hivyo kuwezesha TARURA kufanya kazi vizuri.

**Hongera TARURA,**
**Hongera SAMIA**
**Mungu Ibariki Tanzania.**
**Pascal Mayalla**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Hakika Dunia ni duara!



Na Joseph Kulangwa

**Ni kweli na ndiyo sababu tukatengenezewa kitu aina ya tufe ambacho kina ramani ikituonesha kwetu ni wapi na kwao ni wapi na ukitoka kwenu kwenda kwao utafikaje na lini.**

HISTORIA haidanganyi ingawa wakati mwingine huja na maruweruwe fulani hivi yakatuzuia kuona mbali.

Nakumbuka wakati tunaanza shule tukiwa wadogo, tulifundishwa katika Jiografia kuhusu umbo la Dunia.

Walimu wakitwambia kuwa kuna watu wanadhani pengine Dunia ni kama meza, kwamba ukitembea au ukakimbia kutoka upande mmoja kwenda mwingine, mwishowe utadondoka na hapo utakuwa mwisho wa maisha yako.

Lakini kumbe baada ya uchunguzi na utafiti uliofanywa na wataalamu, ikabainika kuwa Dunia ni duara, kwamba hata utembee na ukimbie vipi, utazunguka na kujikuta umerudi ulikoanzia.

Ni kweli na ndiyo sababu tukatengenezewa kitu aina ya tufe ambacho kina ramani ikituonesha kwetu ni wapi na kwao ni wapi na ukitoka kwenu kwenda kwao utafikaje na lini. Wakasema kumbe pia Dunia inazunguka jua.

Tukaamini walipotwambia kuwa ndiyo sababu kuna mchana na usiku. Mchana ni pale jua linapoimulika Dunia na usiku ni pale jua linapokuwa limetoweka, halionekani.

Walimu wakitwambia jua limezama, huku wazee wakitwambia jua limekwenda kulala.

Tuliwaamini wote, lakini tukijua tu kuwa jua halitembei, bali liko pale pale ila Dunia ndiyo yenye kiherehere cha kulizunguka jua na kusababisha kiza na mwanga, mchana na usiku. Nasi binadamu tukautumia usiku kujipumzisha kwa kulala, isipokuwa wachawi.

Kumbe kiini cha kauli ya Dunia inazunguka ni hicho cha kijiografia, lakini wahenga nao wakatumia kitendo hicho kuasa watu. Ukisikia Dunia inazunguka, ujue kuna mtu umemkosea na anataka kukwambia kuwa ipo siku mtakutana tu.

Wengine wakahanikiza kuwa milima haikutani bali binadamu ndio hukutana. Na iko hivyo kwenye maisha yetu haya mafupi. Kwamba unaweza kukosana na mtu au ukamfanyia roho mbaya, lakini ikaja siku mkakutana mahali usiamini kama ni yeye au ni wewe.

Juzi nchi hii ilitikisika kidogo, kutokana na uchaguzi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wa 'kumrejesha kundini'

Komredi Abdulrahman Kinana, safari hii kama Makamu Mwenyekiti wa Chama hicho upande wa Bara. Ilitikisika, kwa sababu ya jina la huyo mtu, ambaye ni maarufu katika masuala ya kisiasa, akiwa amepitia milima na mabonde mengi. Lakini mimi nimempongeza kwa uvumilivu wake katika masuala hayo.

Hivi fikiria, mtu aliyewaweka madarakani marais wawili wa nchi hii nao wakafanya yao vizuri kwa miaka kumi kumi na kuondoka isipokuwa mmoja ambaye alitumikia kwa miaka sita kwa kudra za Mwenyezi Mungu akanyakuliwa mawinguni.

Mtu huyu aliyechungulia shimoni ilikokuwa inatumbukia

CCM na kufanikiwa kuiopoa na kuirudisha juu ya ardhi, na kuendelea kuongoza na leo anarudi kiroho safi na kuchukua hatamu za kumsaidia Chifu Hangaya kukabiliana na kero za wananchi.

Kumbuka, alivyopata kupitia magumu, akisemwa na kunangwa na watu ambao hata naona chefu kuwataja hapa, nikiwalinganisha na hadhi aliyokuwa nayo Kinana.

Watu hao wakijinasibu kuwa ni ngangari na kumwita majina haya na yale.

Wapo waliomo serikalini, wapo waliomo ndani ya chama, wapo walioko mitaani, lakini kwa kauli na ushauri wa Mzee Yusufu Makamba, atakuwa amewasamehe mara sabini na

kuendelea kusukuma gurudumu la maendeleo chini ya kaulimbiu ya Kazi Iendelee.

Hapo ndipo sasa tunapojua kuwa kumbe kweli Dunia ni duara na siku hazigandi. Sasa wale waliokuwa wakimsema Kinana na kumwita majina, huku wengine wakisema ni mstaafu anawewеseka wanaweka wapi nyuso zao? Wataikumbuka hadithi ya Adili na Nduguze nakuishia kuziba nyuso kwa viganja vyao.

Kwa mchango aliokuwa nao Kinana, ni dhahiri watu walikuwa wanavumilia kusikia alivyokuwa anatwezwa, tena na vijana hao waliokuwa wakiamini kuwa maisha yataendelea kuwa yale yale na vile vile miaka yote, wakishindwa wafanye nini kwa muktadha ule.

Siku zote ni vema mengine kumwachia Mungu, kwa sababu ndiye hupanga yote haya na mengine, ndiyo sababu akampangia Kinana kuwa CCM ni yako tu, utakaa benchi lakini mwishowe utabadili jezi utacheza ukishika nafasi ya kiungo mshambuliaji, Philip Mangula. Na imekuwa hivyo, sasa ni mabao tu!

**Alamsiki!**

# Aliyeua mama yake mbaroni tuhuma za kumuua mke wake

**Na Mwandishi Wetu, MTWARA**

JESHI la Polisi Mkoa wa Mtwara limemkamata Shaibu Kuselela 958), mkazi wa Kijiji cha Lipalwe 'A' wilayani Tandahimba mkoani Mtwara kisha kumfikisha mahakamani kwa tuhuma za kumuua mkewe, Amina Mtausi (40), mkazi wa Lipalwe 'A'.

Akizungumza na waandishi wa habari mjini hapa jana, Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mtwara, Kamishna Msaidizi Nicodemus Katembo, alisema Shaibu anatuhumiwa kutenda kosa hilo mnamo Februari 28, mwaka huu majira yasiyojulikana huko kijijini Lipalwe 'A' kisha mwili wake kuufukia shambani kwao naye kutokomea kusikojulikana.

"Baada ya Jeshi la Polisi Mkoa wa Mtwara kupata taarifa hizo, lilikamilisha taratibu za awali eneo la tukio na kuanza ufuatiliaji kupitia taarifa fiche ili kumpata mtuhumiwa.

"Mnamo tarehe 25.03.2022, mtuhumiwa alikamatwa huko Kijiji cha Mvuleni, Wilaya ya Kilwa mkoani Lindi.

Katika mahojiano amekiri kutenda kosa hilo kwa kumtuhumu marehemu mkewe kumwambukiza magonjwa ya zinaa.

Tayari, mtuhumiwa amekwishafikishwa katika Mahakama ya Wilaya Tandahimba tarehe 01.04.2022 kwa kesi namba PI 2/2022," alisema.

Kamanda Katembo alisema kumbukumbu zinaonyesha kuwa mtuhumiwa aliwahi kumuua mama yake mzazi mwaka 2010 na kutiwa hatiani kwa kosa la kuua bila kukusudia na alihukumiwa kifungo cha miaka mitano jela.

"Jeshi la Polisi Mkoa wa Mtwara linawashukuru wananchi wote kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakiutoa kwani kupitia taarifa fiche ambazo wamekuwa wakizitoa zimesaidia kupambana na uhalifu," alisifu.

Alisema Jeshi la Polisi Mkoa wa Mtwara pia linaendelea kufanya oparesheni za kudhibiti makosa ya usalama barabarani kwa kuwakamata na kuwafikisha mahakani waendesha pikipiki, maarufu bodaboda wanaovunja sheria za usalama barabarani.

"Katika oparersheni iliyofanyika kati ya tarehe 20.03.2022 hadi 01.04.2022, jumla ya pikipiki 300 zimekamatwa kwa makosa mbalimbali. Kati ya hizo pikipiki 140 ziliandikiwa faini na kuachiwa, pikipiki 28 watuhumiwa wake wamefikishwa mahakamani ambapo kesi sita zimemalizika na watuhumiwa kutiwa hatiani.

"Jeshi la Polisi Mkoa wa Mtwara linatoa onyo kali kwa watumiaji wote wa barabara hususani madereva kuzingatia sheria za usalama barabarani. Jeshi la Polisi linaendelea na oparesheni kali ili kuwabani wote wanaokwenda kinyume na sheria hizo na kwamba yeyote atakayebainika atachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria za nchi," alisema.

# CAG aona shida meli bandarini D'salaam

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere, amebaini meli za mizigo zinakaa muda mrefu katika Bandari ya Dar es Salaam na kushindwa kushindana na bandari za nchi jirani huku ikikosesha serikali mapato.

CAG Kichere alibainisha hayo alipokuwa akiwasilisha ripoti ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni 30, 2021 kwa Rais Samia Suluhu Hassan, Ikulu Chamwino.

Alisema Mpango mkakati wa bandari ulikusudia kupunguza muda wa meli kukaa bandarini kutoka siku tatu hadi mbili na kupunguza muda wa kuondoa mizigo kutoka siku 10 hadi tano.

"Nilibaini muda wa meli kukaa bandarini ulikuwa siku tatu hadi sita na kupakua mizigo siku nane na siku 10, baadhi ya mambo yaliyochangia ni utaratibu mgumu wa ujazaji wa nyaraka, kiwango kidogo cha matumizi ya TEHAMA bandarini hali hii inahatarisha fursa bandari ya Dar es salaam,"alisema.

Alipendekeza kuimarishwa kwa mifumo ya TEHAMA ili kurahisisha kazi.




Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya MDH, Dk. David Sando (kushoto), akizungumza katika Mkutano wa Wenyeviti wa Serikali za Mitaa na Watendaji wa Kata, mkoani Dar es Salaam, ulioitishwa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa huo, kupitia Idara ya Afya na Taasisi hiyo juzi, kwa ajili ya kuhamasisha chanjo dhidi ya Uviko- 19. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Bilioni 20/- zatengwa mikopo wafanyakazi

**Na Enock Charles**

KAMPUNI ya Fanikiwa Microfinance imetenga Sh. bilioni 20 kwa ajili ya mikopo kwa wafanyakazi kutoka sekta binafsi ili wajikomboe katika vikwazo vya kiuchumi na kufikia malengo yao.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa bidhaa mpya ya mkopo maalumu kwa wafanyakazi kutoka sekta binafsi mkoani Dar es Salaam jana, Mkurugenzi wa Kampuni hiyo, Nyaswi Makungu, alisema wameamua kuja na bidhaa hiyo baada ya kupata maoni kutoka kwa wadau kutoka sekta binafsi na kufanya tathmini na kuona haja ya kutenga fedha kuwakopesha watumishi hao.

"Tulifanya tathmini na kugundua kwamba kuna baadhi ya wateja tunashindwa kufikia malengo yao kutokana na huduma tunazozitoa," alisema Nyaswi.

Aliongeza: "Bidhaa hii italenga zaidi wateja ambao wameajiriwa na mahitaji ni hati zao za mshahara za miezi mitatu na hicho ndicho kigezo kikubwa na pia kampuni iliyokuajiri iwe inatambulika na inafuata sheria zote za ajira za nchi."

Alisema kampuni hiyo imekuwa ikitoa mikopo kwa watumishi wa umma na wafanyabiashara wadogo, lakini walipofanya tathmini waliamua kuja na bidhaa hiyo kwa wafanyakazi wa sekta binafsi.

Alisema Kampuni hiyo kwa sasa ina wateja takriban 85,000 nchi nzima huku ikiwa na matawi 55 katika mikoa mbalimbali na inatarajia kufikisha wateja 100,000 ifikapo mwishoni mwa mwaka huu.

Kuhusu mkopo huo, alisema Sh. bilioni 20 zimetangwa kwa ajili ya kuwakopesha watu kuanzia kiasi cha Sh. 50,000 hadi Sh. milioni 50 huku riba ikiwa ni asilimia tano na kutarajiwa kuwafikia wateja zaidi ya 5,000 kutoka sekta binafsi.

# MAISHA

APRILI 3, 2022

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

Jumapili




Ukurasa 13

**Miwani giza; chaguo linalopendwa na vijana**



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

Umuhimu wa nyumba kuwa eneo sahihi na tulivu



Ukurasa 12

**HARUSI**




## LAINISHA MIDOMO


# Uonekane mwenye mvuto zaidi

Ukurasa 14

# WATOTO


MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA






| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ■ | G | A | M | B | A |
| ■ | O | ■ | ■ | I | ■ |
| N | M | C | ■ | N | ■ |
| ■ | B | ■ | I | G | A |
| ■ | E | ■ | ■ | W | ■ |
| T | A | M | K | A | ■ |





## PAKA RANGI




## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
APA, OGA, LENGA, PAMBA, BANGUA, PEPONI




Alichokifanya daktari

MTOTO Juma alikwenda kwa rafiki yake Joseph mtaa wa pili. Alipofika alimkuta Joseph akihangaika huko na huku akitafuta kitu.

**Juma:** Habari yako Joseph?

**Joseph:** Sijambo Juma

**Juma:** Aiseee! Nakuona unahangaika uko na kule nini unatafuta?

**Joseph** Dah! Namtafuta mbuzi ambaye nikimpata atakuwa na kibao mama anakitaka.

**Juma:** Hapana mama yako hakumaanisha mbuzi anacho kibao, ila anataka kibao cha mbuzi ambacho kinakuniwa nazi.

**Joseph:** Duuu nimeumbuka.

**SWALI**

Asali inatokana na mdudu anaitwaje?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Mambo ya kung'arisha mafanikio yako!

***KARIBU tena msomaji wangu katika safu yetu hii ya Maisha Ndivyo Yalivyo. Wiki iliyopita nilieleza kwamba huwezi kufanikiwa kwa kufanya kila kitu mwenyewe.***

Nikatoa mifano kadhaa ya watu waliofanikiwa katika maisha kwa kushirikisha watu wengine. Nikamtaja mmojawapo kuwa ni Bill Gates, tajiri mkubwa toka Marekani, mwanzilishi wa kampuni kubwa ya Microsoft.

Vilevile, nikaanza kutaja mambo kadhaa ya kuzingatia endapo unataka kufanikisha malengo yako. Nikasema tafuta washirika waaminifu na watii. Pia tengeneza mfumo madhubuti wa utendaji ambao ukizingatiwa utaleta mafanikio.

Kingine cha kuzingatia ni kwamba, tafuta washirika au marafiki wenye ujuzi na uzoefu. Ili upate mafanikio ni vema kuanza vema, ukikosea mwanzoni itakuwa vigumu sana kujisahihisha baadaye.

Hii itakuepushia makosa mengi hapo mwanzoni na kukupa wepesi wa kuendelea mbele kwa uhakika. Unapokuwa na marafiki na washirika wenye ujuzi na uzoefu itakuwezesha kufahamu mambo mengi kabla hata haujaanza shughuli yenyewe. Hii ni sawa na kufaulu kwa asilimia hamisi tayari.

Inawezekana shughuli unayotaka kuifanya huna ujuzi wala uelewa wa kutosha, hivyo ni muhimu kuwapata wenye sifa kwani hao watakusaidia hata wewe kukupa uzoefu.

Wapo watu wana mtizamo kwamba siyo sahihi kuanzisha shughuli ambayo huna ujuzi au uzoefu nayo. Msimamo huu siyo sahihi kwani lengo siyo wewe kufanya kila kitu mwenyewe. Kumbuka kwamba unalolifanya ni matokeo ya maono Mungu aliyokupa.

Kuna watu walioanzisha biashara ambazo hawakuwa na ujuzi nazo kabisa, lakini walifanikiwa kupata wenye ujuzi wachache wakashirikiana na baadaye kufanikiwa sana.

Jack Ma, aliyeanzisha mtandao wa masoko uitwao Ali Baba, hakuwa na ujuzi wala uzoefu. Alipata washirika wachache wenye ujuzi wa programu za kompyuta na leo amekuwa tajiri mkubwa kuliko wote nchini China.

Huwezi kuwa na ujuzi wa kila fani. Tafuta washirika wenye ujuzi na uzoefu ambao wewe huna na maono yako yatafanikiwa.

Lingine la kuzingatia ili kufanikisha malengo yako ni kutafuta marafiki wenye moyo wa kujitolea. Upo msemo kwamba 'mwanzo ni mgumu' na kwamba bila moyo wa kujitolea utashindwa mapema sana.

Kupata watu walio tayari kujitolea ni changamoto katika ulimwengu ulioweka pesa mbele. Washirika au marafiki wanaoweka pesa mbele hawafai kushirikiana nawe katika maono yako kwani hawa ni mamluki !

Marafiki wa aina hii ni wepesi kuiba na hata kuuza siri za shughuli zako. Watu walioweka fedha mbele hawajali kama shughuli yenu inafanikiwa au la. Tena ni wavivu na wazembe.

Ni kheri kuanza na watu wachache wanaoelewa umuhimu wa kujitolea kuliko kundi kubwa la watu walioweka maslahi yao binafsi mbele.

Wenye moyo wa kujitolea ni wavumilivu huku wakijua kwamba upo wakati wa kupanda, kupalilia, kuweka mbolea na kusubiri mavuno.

Eneo lingine la kuzingatia kufanikisha malengo yako ni kushirikiana na rafiki mwenye ujasiri wa kukwambia ukweli. Ukweli unauma lakini huponya pia. Anayekupenda kweli na kukutakia mafanikio atakwambia ukweli kwa upole na bila kumung'unya. Wengi wetu hatupendi kuambiwa ukweli hasa tunapokosea kwani tunamuona aliyetuambia ukweli kama adui.

Wale unaoshirikiana nao wakiwa na ujasiri wa kusema ukweli na wewe kuwa tayari kusikiliza, utafanikiwa katika maono yako. Usishirikiane na kundi la wanafiki, watu ambao wanalolisema siyo lile wanalolikiri mioyoni mwao.

Jiulize sana aina ya rafiki ambaye kila wakati hukubaliana nawe na kukusifia tu na hata siku moja hakukosoi wala kukusahihisha. Pia tafuta washirika wenye ubunifu. Wapo watu ambao Mungu amewapa vipawa vya ubunifu. Shirikiana na watu kama hao na siyo kuwaonea wivu na kuwakatisha tamaa. Wapo watu waliobuni vitu mbalimbali kwa faida ya nchi yetu lakini hawakusaidiwa kujiendeleza.

Ili maono ya Mungu aliyokupa yafanikiwe, atainua watu wenye vipawa mbalimbali ili ufanye nao kazi. Ingawa maono umepewa wewe haimaanishi una uwezo wa kufanya kila kitu.

Mpenzi msomaji, Waingereza wanao msemo kwamba 'ukitaka kupata rafiki, kuwa rafiki'. Ili kupata rafiki ni muhimu wewe mwenyewe kuwa rafiki. Hali hiyo itawavuta watu wengine kushirikiana nawe.

***Mpenzi msomaji, bila shaka umejifunza jambo hapo. Niishie hapa tukutane tena wiki ijayo panapo majaliwa. Ukiwa na maoni, kisa, tuma ujumbe mfupi kupitia 0715268581.***

## NAWAZA KWA SAUTI
Na Salome Kitomari



# Aliyoyabaini CAG yanakatisha tamaa, yatafutiwe mwarobaini

RIPOTI ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya mwaka 2020/21 iliyowasilishwa kwa Rais Samia Suluhu Hassan, imeonyesha namna gani kuna 'upigaji' mwingi wa fedha za umma kwenye maeneo mengi, hali inayokatisha tamaa wananchi.

CAG hukagua fedha za umma ambazo serikali inawajibika kuzisimamia ipasavyo ili zitumike kwa manufaa ya wananchi wote, badala ya wajanja wachache kujipatia kwa manufaa yao binafsi.

Kila mwaka CAG huonyesha mianya iliyopo kwenye mashirika,taasisi, serikali kuu na serikali za mitaa pamoja na hutoa mapendekezo ya nini kifanyike, lakini hali imeendelea kuwa ile ile na wakati mwingine mbaya zaidi kwa baadhi ya maeneo,jambo ambalo linaonyesha kuna kazi kubwa ya kufanya.

Baadhi ya mamlaka zimeshindwa kutengeneza taarifa zake inavyotakiwa au kukosekana viambatanisho na nyaraka muhimu za matumizi ya fedha ya Watanzania.

Kila Mtanzania analipa kodi kwa namna yake, kwamba kuna mwenye biashara, kampuni,mfanyakazi au mjasiriamali ambao viwango vya kodi hutofautiana kutoka mmoja kwenda mwingine, lakini unaponunua bidhaa lazima utalipa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT); maana yake kila mmoja anawajibika kulipa kodi na ana haki ya kunufaika na kodi hiyo kupitia huduma bora za kijamii.

Katika ukaguzi huo, kati ya taasisi za umma 999 zilizokaguliwa mwaka 2020/21, zipo zilizopata hati zenye shaka na zingine CAG alishindwa kutoa maoni.

Alimweleza Rais Samia kuwa walikagua mifuko ya hifadhi ya jamii ya NSSF na PSSSF wakabaini mafao ya pensheni yanazidi mapato yatokanayo na michango ya wanachama.

Aidha,vyama vya siasa vilivyokaguliwa vilivyopata hati zenye shaka ni CUF ,UDP, SAU huku hati chafu ni ADC,CHAUMMA,UMD,TLP na Chama Cha Demokrasia Makini huku akishindwa kutoa maoni kwenye hesabu za AFP.

Kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa, walibaini Sh.bil 47.07 zilizokopeshwa kwa wanawake,vijana na wenye ulemavu hazikurejeshwa.

Hili ni jambo la kusikitisha kwa kuwa fedha hizi kama hazikutumika basi zilipaswa kurejeshwa ili wakopeshwe wengine na kuona thamani ya fedha kwa kuangalia mabadiliko kwa waliokopeshwa, lakini kwa kutorejeshwa inaonyesha kuna tatizo mahali, hivyo lazima lishughulikiwe.

Mathalani,wakati wa Mkutano wa Sita wa Bunge, baadhi ya wabunge walisema mikopo hiyo inashindikana kurejeshwa kwa kuwa waliokopeshwa siyo wanufaika, bali kuna watu wameunda vikundi na kuzichukua huku wakitaka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kuchunguza.

Fedha hizo zinatukumbusha mabilioni ya JK (Jakaya Kikwete) ambazo zilitolewa kwa kila mkoa kukopesha makundi maalum ziliishia 'kupigwa' kiasi cha lengo kutofikiwa.

Aidha, CAG alisema halmashauri 83 hazikuchangia Sh. bilioni 6.68 ya asilimia 10 ya bajeti yao kwa mujibu wa sheria kwa ajili ya kusaidia makundi hayo kubadilisha maisha yao.

Pia,alibaini halmashauri zilifanya malipo ya Sh. milioni 556.84 kwa wastaafu waliofariki,kutoroka,kuacha kazi na waliokuwa likizo.

Aidha,alibaini matumizi yasiyo na manufaa yaliyofanyika kwa bidhaa ambazo hazijawahi kutolewa, huku kukiwa na matumizi ya fedha mbichi (fedha ambazo hazijapelekwa benki) zaidi ya Sh. bilioni 17 kwa halmashauri 147.

Kwa ujumla huu ni upigaji ambao kimsingi unakatisha tamaa walipakodi wa nchi hii, ambao wanataka kuona fedha wanazolipa zinasimamiwa vyema, zinafanya kazi zinazotakiwa na siyo watu wachache kuzifanyia ubadhirifu na kunufaika wakati wengi wanaumia.

Fedha zilizoibwa zingeweza kununua vifaa tiba, dawa na kujenga majengo ya zahanati, vituo vya afya na hospitali. Pia zingeongeza miundombinu ya shule na barabara, ili Watanzania wote wanufaike na keki ya taifa, lakini zinapigwa na wachache kwa manufaa ya wachache.

Ni muhimu walipakodi wakaona uwajibikaji wa wazi wa kila shilingi yao; kwamba watu wakamatwe na kufikishwa mahakamani, lakini mali walizozipata kwa njia haramu zifilisiwe kwa kuwa wametudhulumu Watanzania licha ya imani tuliyokuwa nayo kwao.

Bila hatua madhubuti kuziba mianya ya upotevu wa mapato, hali itaendelea kuwa hii ambayo itakatisha tamaa, itaonekana serikalini ni shamba la bibi kwamba mtu anaweza kuingia kwa ujanja wake akachota fedha akazitumia na kuendelea na maisha kama kawaida.

Bila kudhibiti mchwa hawa, Watanzania watakata tamaa itaonekana fedha za umma ni shamba la bibi kila mtu anavuna atakavyo, hivyo ni muhimu kuona uwajibikaji kwa waliopewa dhamana ya kusimamia fedha na rasilimali za umma kwa niaba ya watu takribani milioni 60.

Lazima kujenga misingi imara ya kukomesha upigaji wa mali za Watanzania ambayo ingepaswa kuwanufaisha kupitia huduma za kijamii kama afya,elimu,maji na miundombinu.

Kila kikao cha Bunge,kwenye maswali na majibu wabunge huwasilisha kilio cha wananchi wao mengi hujikita kwenye Wizara inayohudumia wananchi moja kwa moja TAMISEMI, wakitaka kujua lini barabara fulani itakamilika, lini zahanati,kituo cha afya au hospitali itapata vifaa tiba na dawa, lakini majibu huwa fedha zinatafutwa au mchakato unaendelea.

Kama kuna fedha zinapotea ambazo zingeweza kutatua changamoto hizo inamaanisha kwamba lazima hatua zichukuliwe kuhakikisha mianya ya wizi, ubadhirifu na ufujaji wa rasilimali za umma inazibwa, ili kila Mtanzania afurahie kulipa kodi kwa kuwa fedha yake itakuwa salama na inaonekana inafanya nini.

# HARUSI







Shangwe na vigelegele vilitawala kwa ndugu, marafiki na jamaa wa familia ya Mkele baada ya mtoto wao Faraji Mkele kuamua kufunga ndoa na Fatma Mwandolo. Harusi hiyo ilifanyika Machi 25 mwaka huu Mbagala Mangaya, kisha iliandaliwa sherehe ya kuwapongeza iliyofanyika Mtoni Azimio jijini Dar es Salaam.

# MITINDO

## MIWANI YA GIZA







# Chaguo linalopendwa na vijana

MIWANI ni miongoni mwa mapambo yanayopendwa kuvaliwa na wanaume kwa wanawake kama pambo la kuongeza mvuto.

Wanaume wanaongoza kwa uvaaji wa miwani kuliko wanawake, hivyo wabunifu wamechukua nafasi hiyo kwa kubuni na kutengeneza aina mbalimbali za miwani ya kuvutia. Kwa ujumla miwani ipo ya aina mbalimbali, lakini leo tutazungumzia jinsi ya kutumia ile yenye kioo cha giza maarufu kama miwani ya jua.

Wataalamu wa masuala ya mitindo wanasema mwanaume anapovaa miwani ya jua, anakuwa na muonekano wenye kuvutia na ushawishi wa kimahaba.

### JINSI YA KUCHAGUA

Kabla ya kuamua kutumia miwani ya jua, hakikisha unafanya chaguo sahihi la mavazi yanayolingana.

### UKUBWA

Hakikisha ukubwa wa miwani iwe sawa na aina ya kichwa chako, usichukue mikubwa au midogo sana kwa sababu hayatakukaa vyema na kukupa muonekano tofauti na ulivyotarajia.

### MITINDO

Baadhi ya wanaume wanavaa miwani bila kuangalia aina gani ya mitindo inayofaa, jambo hili linaelezwa ni baya kwa sababu mitindo mingine haifai kuvaliwa mbele ya jamii. Unashauriwa kabla ya kuchagua hakikisha unapata ushauri wa kutosha kutoka kwa mtaalamu au muuzaji.

### NYAKATI


Miwani ya jua imegawanyika katika aina tofauti kulingana na vipindi itakavyotumika. Kama unataka kutumia sehemu yenye mwanga mkali hasa mchana, unatakiwa kuvaa kioo cha kiza, sehemu yenye uono hafifu kama usiku ni vyema ukavaa yenye kioo chenye weusi angavu.

Hapa wengi wanaonekana vituko kwani mara nyingi watu wanajikuta wakivaa miwani yenye kiza nyakati za usiku, hivyo huwasababishia kero na mtazamo tofauti kwa jamii.

### NGUO

Kwa wale wanaopenda kuwa na flemu zenye rangi tofauti, unatakiwa kuhakikisha rangi za flemu zilingane na nguo unazotaka kuvaa kwa wakati huo.

UREMBO



LAINISHA MIDOMO

# Uonekane mwenye mvuto zaidi

WATU wengi hasa wanawake wanapenda kuwa na midomo laini yenye mvuto wa kimahaba.

Lakini kutokana na asili ya mtu na hali ya hewa, vimepelekea wengine kuwa na midomo migumu isiyovutia hasa katika swala zima la mahaba.

Hata hivyo kama wewe ni mwathirika wa tatizo hili na kwa maana nyingine hata imekupelekea kuzikatia tamaa lips zako.

Kuna njia za asili na kisasa za kutengeneza midomo katika mwonekano wa kuvutia,

**KUNYWA MAJI MENGI**

Ukosefu wa maji mwilini si mzuri kwa afya ya ngozi yako. Njia nzuri ya kukuza afya ya ngozi yako ni kwa kunywa maji mengi kila siku.

Hii itakusaidia kuboresha ngozi yako, kukuza seli mpya na kuweka ngozi yako hali ya unyevu.

Sugua midomo kwa Tango

Kusugua midomo yako kwa kutumia vipande vya tango, itasaidia kulainisha na kuzing'alisha lips zako. Matango yana kemikali asilia aina ya phytochemicals ambayo itasaidia kulainisha na kunyevua midomo yako.

**TUMIA MAFUTA YA NAZI**

Mafuta ya nazi yana matokeo mazuri sana katika ngozi ya mwanadamu.

Paka kiasi kidogo tu cha mafuta ya nazi kwenye midomo yako itasaidia kulainisha na kuiweka midomo yako katika hali ya kuvutia.

**PAKA MAFUTA YA PETROLEUM JELLY**

Kupaka mafuta ya petroleum jelly muda mfupi kabla ya kwenda kulala itasaidia kunyevua midomo yako.

Ukijiwekea mazoea ya kufanya hivi kwa muda mrefu, itakusaidia kuongeza ulaini wa midomo yako na kuifanya kuwa na muonekano wa kuvutia sana.

**TUMIA RANGI YA MIDOMO**

Rangi ya midomo maarufu kama 'Lipstick' za kunyevua midomo zinasaidia kulainisha midomo yako, lipstick hizo zimetengenezwa kwa siagi ya kakao, siagi ya shea na mafuta ya nazi ambayo husaidia kulainisha midomo yako.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Wali wa korosho na mbogamboga

KAMA wanavyosema wahenga kuwa mchele ni mmoja mapishi mbalimbali.

Mchele unaweza kupikwa mapishi aina tofauti ambayo tumezoea kuona, lakini ni vyema ukawa mbunifu ukapika aina mpya ya pishi.

Leo katika safu hii tutaelekezana namna ya kupika wali wa mboga uliochanganywa na korosho.

Wote tunafahamu utamu wa korosho sasa uchanganye na pilau itakuwaje.

**MAHITAJI**

Kilo moja ya wali uliopikwa, mchanganyiko wa mboga majani upendazo, gramu 250 za korosho, kitunguu saumu na tangawizi mbichi.

Osha na katakata viungo, mafuta ya kupikia, vijiko viwili vya Soy Sauce na chumvi.

**NAMNA YA KUANDAA**

Andaa kila kitu na kiwe karibu na kikaangio chako kisha washa moto meko yako ili kikaango kipate moto.

Weka mafuta ya kupikia kisha weka korosho na kaanga ziwe na rangi ya kahawia kabla ya kuziepua na kuziweka pembeni.



Kama utatumia nyama ya ng'ombe, mbuzi au minofu ya kuku, unaweza kukaanga pamoja na korosho hizi ili ziive pamoja.

Katika kikaangio, weka kitunguu, tangawizi, na kitunguu saumu halafu kaanga kiasi.

Sasa ongezea ule mchanganyiko wa mboga ulizozichemsha na kisha ukazichuja. Kaanga kwa muda wa dakika moja.

Ongeza soy sauce pia na ukaange kwa muda wa angalau sekunde 15. Sasa ni zamu ya kuongezea ule wali wako uliopo tayari.

Hapa unaongezea korosho pia kama unatumia nyama ongeza pamoja na nyama endelea kuchanganya ichanganyike vizuri.

Unaweza mwagia juu ya wali wako majani mabichi ya kitunguu na majani ya giligilani ili kuongeza ladha na muonekano wa rangi tofauti.

Waliwako utakuwa tayari kuliwa wakati wa mchana au usiku.

MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya



## Jinsi ya kupamba meza ya chakula



NI jambo rahisi kuandaa meza wakati wa chakula, lakini kwa baadhi ya watu wana changamoto ya kufahamu namna ya kupamba baada ya chakula.

Wakati wote ambao haitumiki, meza inatakiwa kuwa na mvuto wa kipekee ili kumfanya mtu kuvutika na kuona mandhari ya kupendeza.

**1:** Wakati unapokuwa umekaribisha watu nyumbani kwa chakula, ni rahisi kupendezesha meza kuendana na mandhari, rangi au hata majira ya tukio kama labda ni kipindi cha sikukuu fulani za mwaka.

**2:** Pambo moja kubwa katikati ya meza ni moja ya njia ya kuipendezesha ambayo imekuwa ikitumika tangu enzi. Pambo liwekwe katikati ya taa ya kuning'inia juu ili kutoa nakshi nzuri.

**3:** Tumia trei kama hauna pambo moja lenye ukubwa wa kutosha kuendana na ukubwa wa meza, tengeneza muonekano wa kitu kikubwa kwa kukusanya vitu vidogo pamoja kwenye trei.

**4:** Utepe wa meza unaweza kuupamba kwa staili mbili ya kwanza ikiwa ni utepe pekee na ya pili ni utepe na mapambo juu yake.

Tumia zile mati za kuwekea sahani hata kama sio wakati wa kuandaa chakula.

# Umuhimu wa nyumba kuwa eneo sahihi na tulivu

MIONGONI mwa maeneo ambayo huwa ni faraja na ya kupumzisha akili baada ya shughuli nyingi ni nyumba yako.

Nyumbani ndipo palipo na mkusanyiko wa maisha, kumbukumbu na upendo kwa asilimia kubwa ya watu.

Binadamu kila mmoja hujishughulisha na mambo mbalimbali lengo likiwa ni kujitafutia ridhiki na kuhakikisha mkono unakwenda kinywani na mambo mengine ya kifamilia yanakwenda sawa.

Lakini pamoja na kujishughulisha huko, mwisho wa siku lazima arejee nyumbani kujipumzisha bila kujali umbali wake.

Hivyo basi, kwa vyovyote vile lazima uhakikishe nyumbani kunakuwa mahali sahihi, panapokupa furaha, amani na utulivu.

Si tu kwa utulivu, ni muhimu kuzingatia kwamba nyumba hiyo ya kuishi iko eneo ambalo halitakusababishia karaha, kuanzia aina ya watu wanaokuzunguka, madhari yake, ufikikaji wake na vitu vingine muhimu.

Utulivu huo si tu kwako, bali na kwa familia yako kwa wale wenye nazo.

Watu wengi hasa tunaopanga, huwa tunakosa utulivu tunapotafuta nyumba za kupanga kutokana na kutokujipa muda wa kutosha kutafuta nyumba hizo na hivyo wakati mwingine tunajikuta katika wakati mgumu baada ya kuhamia kwenye nyumba ambazo baadae hubaini kwamba aidha hazikuendana na sisi au nyumba zinaendana nasi lakini mazingira yanayozunguka nyumba ndio siyo rafiki.


Na kwa sababu hiyo, watu wengine hulazimika au kutamani kuhama kwenye nyumba ndani ya muda mfupi hata kama pesa ya pango waliyolipia haijaisha.

Mojawapo ya vitu vinavyosababisha watu watamani kuhama kwenye nyumba kabla ya wakati ni pamoja na aina ya majirani wanaowazunguka, kwamba baadhi yao ni wakorofi mpaka kufikia hali ya kukosesha amani na utulivu, kwamba kila siku migogoro haiishi, wanaanzisha jipya kila wakati.

Hata mwenye nyumba mwenyewe anaweza kuwa chanzo cha wewe kutamani kuhama nyumba yake kwa sababu ya 'chokochoko'zake za hapa na pale, au ukahamia lakini ukabaini kwamba eneo iliyopo nyumba kunafanyika mambo ambayo yako kinyume na wewe au na imani yako, kwa hiyo ikakukosesha amani.

Kutokufanikiwa kutimiza ndoto ya kuishi kwenye nyumba zilizo katika mazingira yanayoendana nasi kunasababisha hata ufanisi katika utendaji kazi wakati mwingine kupungua, wakati wote mtu anawaza atakumbana na lipi jingine jipya au kutokuwa na uhakika na amani ya familia yake. Kwa hiyo ni muhimu kuishi kwenye nyumba zilizo katika mazingira yanayoendana na sisi.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2022
SMS - 0621 412 879
JUKWAANI
NYIE SI JEURI? NAPITA BARABARA YENYE MAROLI TUONE!
DEREVAAAA! BASI TUNALIPA USITUPITISHE HUKO!
CHONDE BABA TUNA ROHO!
HUWEZI KUNIHUDUMIA HUKU UMEGANGAMALA KAMA MJESHI NA GWARIDE! KAMA HUWEZI KULEGEA NA KUNYUMBULIKA SILIPI!
HUYU HAJAWAHI KUZIONA HIZI SAMPULI TOKA KANDA MAALUM!
UKIIENDEKEZA NYUMBA NDOGO SAFARI YA MOTONI NYEPESI MNO!
KITAA CHA KWETU
NDANI YA KIBASI
NASEMA HIVI!! MSIPOBADILISHA JINA LA MTAA KUWA JINA LANGU NAUA MTU!
JAMANI MAJINA YA MITAA YAME-BATIZWA NA 'POSITIKODI' SIO SISI MNATUONEA!
SIRIKALI ZA MITAA
HIVI WE DEREVA HUONI KAMA UNAHATARISHA MAISHA KUSHINDA HUMU KWENYE GARI BOVU?
HUMU KUNA HELA NAPIGA TRIPU KUTWA NZIMA, NAMDANGANYA TAJIRI LIMEKAMATWA KUTWA NZIMA, HABISHI
NAOMBA NAMBA YA TAJIRI YAKO NIENDE HEWANI NAJISIKIA KUMPA HUU UBUYU!
HAKOLEI UBUYU WALA UKWAJU, TUSHAMPIGA 'ZONGO'
UGOMVI WA BAR HUUWEZI NDUGU, UMEGOMBANIWA KAMA PILAU LA SHUGHULI! DUH!
USINICHOKONOE HAPA NILIPO SINA UHAKIKA KAMA SIJACHOMOLEWA 'FIGO'
WE BHANA KAZA ROHO! NI KWELI NIMEMKAMATA MKEO NA BWANA, LAKINI KASEMA NISISEME! 'WAKANIKATIA FUNGU' SHETANI KAWAACHIA!
'GHOSH!' KAMLETE SHETANI
...KINYUNYIZO CHA LEO...
...UGOMVI WA NDUGU INGILIA UONE!

# Wanajeshi wa Russia wazidi kuondoka Kyiv

## ■Miji mingine yaendelea kushambuliwa

**KYIV,** UKRAINE

RAIS wa Ukraine Volodymyr Zelensky, amewaonya watu wake kuwa makini na wanajeshi wa Russia, ambao wanaondoka baada ya kuuzingira mji mkuu wa Kyiv zaidi ya mwezi mmoja.

Alisema kuondoka kwao wanatengeneza mazingira ya maafa nje ya mji huo kwa kutega mabomu ya ardhini karibu na nyumba na miili ya watu waliokufa.

Kiongozi huyo alisema mapema jana kuwa wanajeshi wa Russia wanaondoka katika maeneo yao kutokana na kushindwa malengo yao ya kuutwaa mji huo.

Wakati huo huo, mzozo wa kibinadamu katika mji uliozingirwa wa Mariupol unaendelea kupamba moto baada ya wanajeshi wa Russia kuzuia operesheni ya kuwahamisha watu kwa siku ya pili mfululizo.

Mapambano yaendelea Mariupol

Katika mji wa kusini wa Mariupol, wakazi waliofanikiwa kukimbia mashambulizi ya makombora kwa wiki kadhaa walisimulia uharibifu mkubwa waliouacha nyuma. Walisema mji huo sasa ni kaburi la pamoja kwa kila mtu. Takribani watu 160,000 bado wamenasa Mariupol, wakisubiri msaada kwa sababu hawana maji, chakula wala umeme.

Rais Zelensky alikutana Kyiv na Rais wa Bunge la Ulaya Roberta Metsola

Askari wa Russia wameuzingira Mariupol katika jaribio la kuukamata mji huo ili kuunganisha na maeneo yaliyojitenga katika mikoa ya Luhansk na Donetsk chini ya askari wanaoungwa mkono na Moscow katika upande wa mashariki na rasi ya Crimea, ambayo ilichukua mwaka wa 2014.

Shirika la Kimataifa la Msalaba Mwekundu, ambalo timu yake ya wahudumu tisa katika magari matatu walikuwa njiani kwenda mjini humo kusaidia kuratibu operesheni ya uokozi, walisema walishindwa kufika Mariupol wala kusimamia uhamishwaji salama wa raia.



Polisi akimwangalia mbwa mbele ya wanajeshi wa Ukraine waliokuwa mstari wa mbele wa mapigano mashariki mwa Kharkiv jana. Vikosi vya Russia vimeripotiwa kurudi nyuma katika baadhi ya miji ya nchi hiyo. **PICHA: AFP**

**MAZUNGUMZO YAMEKWAMA BAINA YA UKRAINE NA URUSI**

Kwenye uwanja wa mapambano, wanajeshi wa Ukriane walianza kuchukua tena udhibiti wa baadhi ya maeneo yakiwemo ya karibu na mji mkuu Kyiv na eneo la kusini la Kherson, mji pekee muhimu ambao Urusi ilikuwa imeukamata.

Wizara ya ulinzi ya Ukraine ilisema wanajeshi wa Russia wanaendelea kutekeleza mpango wao wa kuondoka katika baadhi ya maeneo kuanzia kaskazini mwa Kyiv kuelekea mpaka wa Belarus. Raia wanaendelea kuondoka katika maeneo yaliyoharibiwa kwa vita wakati askari wa Ukraine wakivikomboa vijiji 11 katika maeneo ya karibu na Kyiv na Cherginiv katika upande wa kaskazini.

**UINGEREZA YAZUIA NDEGE NYINGINE**

Serikali ya Uingereza imesimamisha kuruka ndege inayohusishwa na Russia, Waziri wa Uchukuzi Grant Shapps ameandika kwenye ukurasa wa Twitter.

Ndege hiyo ilizuiwa kupaa kutoka Uwanja wa Ndege wa London Luton, ambako imebaki ili Idara ya Uchukuzi ifanye uchunguzi iwapo ilikiuka vikwazo vilivyowekwa vya kupiga marufuku ndege zinazohusishwa na Russia.

Maofisa hawakutoa taarifa yoyote kuhusu jina la mmiliki wake wakati uchunguzi ukiendelea.

Idara ya Uchukuzi hivi karibuni imeweka kizuizini ndege mbili za binafsi za Eugene Shvidler, mshirika wa Roman Abramovich, pamoja na helikopta ya binafsi inayomilikiwa na HeliCo Group LLC.

**UKRAINE YAJIANDAA KWA VITA VYA KEMIKALI**

Imeripotiwa kuwa Marekani imekuwa ikituma vifaa vya kinga (PPE) kwa Ukraine kutokana na ombi la nchi hiyo ili kujiandaa kwa shambulio lolote la silaha za kemikali wakati wa vita.

Msemaji wa Baraza la Usalama la Kitaifa la Rais Joe Biden, alithibitisha kwamba vifaa vya kuokoa maisha vimetumwa nchini humo.

PPE inadhaniwa kujumuisha barakoa za gesi, suti za hazmat na vifaa vingine.

Ni kiasi gani ambacho Marekani inapanga kutuma haikufahamika mara moja, lakini msemaji huyo alisema msaada huo hauhatarishi utayari wetu wa ndani.

Marekani na Russia zimerushiana tuhuma katika wiki za hivi karibuni kwamba silaha za kemikali na silaha za kibaiolojia zinaweza kutumwa.

Maofisa wa Marekani wanahofia kuwa Russia inaweza kuwa inapanga operesheni ya uwongo ya bendera kuhusu matumizi ya silaha hizo.

**MAREKANI YAAHIDI NYONGEZA YA MSAADA**

Wizara ya Ulinzi ya Marekani imetangaza kutenga kiasi cha kitita cha Dola milioni 300 kama msaada wa usalama kwa Ukraine ili kuimarisha uwezo wa ulinzi wa nchi hiyo.

Nyongeza hiyo ni kiasi kingine cha Dola bilioni 1.6 ambacho taifa hilo lilikiahidi kukitoa tangu Russia ilipoanza uvamizi wake Februari mwaka huu.

Taarifa ya msemaji wa wizara hiyo John Kirby, ilisema hatua hiyo inaonesha usisitizwaji wa dhamira isiyotetereka ya Marekani kwa taifa la Ukraine katika kulinda uhuru wake wa kimipaka.

Jumatano iliyopita Rais Joe Biden, na kiongozi wa Ukraine,Volodymyr Zelensky, walijadiliana juu ya nyongeza ya msaada wa ziada katika kulisaidia jeshi la Ukraine.

Taarifa hiyo ilitolewa na Ikulu la Marekani baada ya mazungumzo hayo kwa njia ya simu.

**WATU 3,000 WAMEONDOLEWA MARIUPOL**

RAIS wa Ukraine,Volodymyr Zelensky, alisema watu takriban 3,000 wameondolewa salama katika mji uliozingirwa wa Mariupol.

Kupitia hotuba yake kwa njia ya video, alitangaza kutimizwa kwa makubaliano kwa njia salama ya kuondoka kwa wakimbizi katika mikoa mitatu ya Donetsk, Luhansk na Zaporizhzhia.

Alisema katika hatua hiyo wamefanikiwa kuwaokoa watu 6,266, wakiwemo 3,071 kutoka Mariupol.

Jana jioni, mwandishi wa shirika la habari la Ufaransa AFP alisema alishuhudia mabasi 30 yakitoka katika mji wa Zaporizhzhia, miongoni mwa hayo yalikuwa yamewapakia watu kutoka Mariupol na kupelekwa katika maeneo ambayo yanadhibitiwa na serikali ya Ukraine.

Hata hivyo haijawa wazi kama Zelensky alikuwa anazungumzia idadi hiyo ya watu au la. Lakini Naibu Waziri Mkuu wa Ukraine Iryna Vereshchuk, alisema kuna njia saba za uokozi zimepangwa kutoka katika maeneo yaliyozingirwa.

## MAKALA

# KUCHAGULIWA KWA KINANA MWELEKEO MPYA WA CCM



**Na Magabilo Masambu - 0689157789**

MACHI 31, 2022, Halmashauri Kuu ya CCM taifa ilipitisha jina la ndugu Kinana aliyewahi kuwa Katibu Mkuu wa chama hicho, kugombea nafasi ya makamu mwenyekiti bara. Nafasi ambayo iliachwa wazi na mzee Philip Mangula, baada ya kung'atuka kwenye nafasi hiyo.

Aprili Mosi Mkutano Mkuu Maalum wa CCM taifa ukamchagua rasmi Mzee Kinana kuwa makamu mwenyekiti Bara.

Binafsi naona kuchaguliwa kwa Mzee Kinana kutatoa mwelekeo mpya wa siasa ndani ya chama na siasa za nchi kwa ujumla. Tutakumbuka wakati Mzee Kinana akiwa katibu mkuu wa CCM, ndiyo wakati ambao siasa za nchi hii zilikuwa zenye ushindani wa hoja kuliko kipindi kilichofuata baada yake.

Kipindi kilichofuata kukaonekana kukosekana kwa demokrasia kwanza ndani ya chama chenyewe, lakini pia kwa nchi kwa ujumla.

Ni ukweli uliowazi kwamba, kuna kipindi chama kilipitia wakati mgumu japo haikuwa inaelezwa na hasa baada ya kufanyika mabadiliko madogo katika katiba ya chama chenyewe, mabadiliko ambayo wengi walisema yalikuwa yanafanya chama kiwe na hati miliki ya baadhi ya watu ndani ya chama hicho, nafikiri katika mkutano wa juzi pamoja na mambo ya uchaguzi, lakini umeenda sambamba na marekebisho ya katiba ya chama ambayo ni matokeo ya mabadiliko yaliyofanyika, katika awamu iliyopita chini ya mwenyekiti wake, John Magufuli.

Sina wasiwasi na uzoefu wa Mzee Kinana, kwa sababu kwa taaluma tu inaelezwa kwamba ni msomi katika Sayansi ya Siasa, anao uzoefu wa siasa za ndani na za kimataifa ameshika nyazifa nyingi ndani ya nchi hii, zaidi ya yote ni muumini wa demokrasia kama alivyobainisha katika hotuba akiwa makamu mwenyekiti mpya bara.

Kutokana na uzoefu wake kama nilivyoeleza hapo juu, sisi kama Watanzania tunatarajia atoe mwelekeo mpya wa siasa zetu za ndani, yeye binafsi ameweka wazi kwamba chama hakitakiwi kuwa hati miliki ya mtu ndivyo hivyo hata nchi haitakiwi kuwa miliki ya mtu au kikundi cha watu wachache bali kama ambavyo chama ni cha wanachama na wasio wanachama.

Hata nchi inapaswa kuwa ya watanzania wote kila mmoja anapaswa kutoa mchango wake wa maendeleo kwa nchi.

Kwahiyo chini ya uongozi wake tunatarajia aweke uwanja sawa katika kuhakikisha shughuli zote za kijamii na kisiasa zinafanyika kwa usawa, kama ambavyo ilikuwa kuanzia mwaka 2015 kurudi nyuma kipindi ambacho vijana wengi walijihusisha na siasa kwasababu walikuwa na uhuru mkubwa wa kuzungumza wakaonekana.

Mzee Kinana katika hotuba yake fupi amegusia uimara wa chama. Nami naungana naye kwamba, taasisi imara huwa ni bora zaidi kuliko watu imara, ukijenga taasisi imara inajisimamia, inajitetea na inajiendesha hata ikipata watu dhaifu bado itasimama. Chama cha Mapinduzi kinatakiwa kusimama chenyewe bila usaidizi wa taasisi nyingine yoyote ni chama kikubwa na kikongwe, kina uwezo wa kujitetea chenyewe bila usaidizi na hayo ndiyo mawazo ya mzee Kinana nami namuunga mkono mia kwa mia.

Uchaguzi wa Mzee Kinana kuwa makamu mwenyekiti si kwamba tu utatoa mwelekeo mpya lakini pia, naamini umekuwa na funzo kubwa sana katika siasa zetu ndani ya vyama na nchi kwa ujumla. Nilichogundua ni kwamba siasa ni kama gwaride, unaweza kuambiwa nyuma geuka ukajikuta uliyekuwa umetangulia ukawa nyuma na aliyekuwa nyuma akawa mbele!

Kuna umuhimu mkubwa kuweka akiba ya maneno, tunapokuwa kwenye siasa au hata maisha ya kawaida tu, kwa hali ilivyokuwa wakati fulani haikutegemewa kama baadhi ya watu leo wangelikuwa tena mahala fulani lakini imekuwa, kazi yao kubwa sasa si kulipa visasi kama alivyoshauri mzee Yusufu Makamba lakini liwe fundisho kwa kila mtu.

Maisha hayana fomula, tunajua tulikotoka hatujui tuendako.Tunapopanda ngazi, tuwaheshimu sana walioko chini maana tutawahitaji wakati wa kushuka.

Katika makala zilizopita nimewahi kushauri kwamba CCM imara inahitaji upinzani imara, huwezi kujiona imara kama unadhoofisha mshindani wako kwa njia zisizo sahihi, kufanya hivyo ni kujidhoofisha mwenyewe pia, maana mwisho wa siku utalala na kujiona umeshinda kumbe katika uhalisia unakuwa dhaifu.

Chini ya uongozi wa Mzee Kinana naiona CCM yenye kutumia hoja kujijenga na siyo kutumia nguvu na hii itatoa nafasi kwa makada wa chama ambao walibweteka huku wakiamini kwamba, kuna watu fulani watafanya kazi hiyo.

Naziona siasa za ushindani wa kistaarabu na pengine tutarajie katika uchaguzi mkuu ujao wa mwaka 2025, kuwa na bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lenye mchanganyiko wa wabunge wa kila aina, kuliko bunge la sasa lenye muelekeo wa chama kimoja.

Tunataka wabunge watowane jasho, ili ambao hawana uwezo waonekane. Bunge la chama kimoja ni kichaka cha wabunge dhaifu au wasiojua chochote kuhusu masuala ya siasa na uongozi wa nchi, wanajificha kwenye makofi ya jumla, tunataka ifike mahala ushindani uwachambuwe wanaofaa na wasiofaa maana wataonekana katika kujenga hoja na hilo halitaonekana ikiwa bunge lina wabunge wa chama kimoja, tutakuwa na wabunge wa posho na mishahara.

Mwisho. Nina imani na mzee kinana, kwamba atajenga chama ambacho kila mtu atakuwa na nafasi ya kujiona binafsi kwamba anafaa kuwa kiongozi, chama kitakacho waunganisha wanachama wote bila misingi ya ukanda, ukabila, udini na kila aina ya ubaguzi.

Chama kitakachopewa nafasi sawa kwa vyama vingine kufanya siasa, ili chenyewe pia kiweze kujipima ni wapi kipo. Zaidi chama kitakachowafanya wanachama wake wawe ni wenye furaha na uhuru wa kutoa maoni ndani ya chama na nje ya chama pia. Nikutakie utumishi mwema na siyo utukufu mwema Komredi Abdulraman Kinana.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**ARUSHA-TANZANIA**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Unavikumbuka vipindi vya Redio Tanzania?



**Na Adam Fungamwango**

HIVI sasa kuna stesheni nyingi sana za redio kutokana na mabadiliko ya teknolojia na wakati pia. Kuna televisheni kibao, lakini pia zipo televisheni na redio za kwenye mitandao maarufu kama 'on line.'

Kama yote haitoshi kuna mitandao mbalimbali ya kijamii. Hii inafanya kila mtu kuchagua kile ambacho anataka kusikiliza au kuangalia kwa wakati huo. Kila mtu anasikiliza kivyake. Haikuwa hivyo kabla na baada ya uhuru. Nchi ilipopata uhuru, miaka michache baadaye, kukawa na redio moja tu ambayo iliitwa Redio Tanzania Dar es Salaam. Umaarufu wake iliitwa (RTD).

Hakuna Mtanzania aliyekwepa kusikiliza kipindi chochote kile kinachorushwa na redio hiyo. Ni kwa sababu hakukuwa na redio nyingine. Utake usitake utasikiliza. Labda ukichoka ufunge, hadi wakati wa kipindi unachokipenda.

Ni redio ambayo msingi wake mkubwa ilijenga umoja, mshikamano, kupendana, kulinda maadili ya nchi na utamaduni wa Mtanzania. Kingine ni kutoa elimu na kuburudisha.

Ndiyo miaka ambayo anachokisikiliza Mtanzania wa Kigoma, ndicho anachokisikiliza wa Pemba. Wa Mtwara akisikiliza kitu, basi wa Arusha naye ni hicho hicho. Ndiyo maana Watanzania wa miaka hiyo hadi leo wanazungumza lugha moja. Anachokijua wa Shinyanga, ndicho hicho anachokijua wa Ruvuma. Kwa sasa unaweza kukitaja kipindi fulani cha kwenye redio mwingine akakwambia kuwa hakifahamu.

Lakini wakati ule ni lazima akifahamu, ndiyo maana leo nimekuja na mada ya vipindi vya wakati huo ambavyo vitawakumbusha mbali wengi kwa sababu hakuna ambaye atasema havijui kwani kila mmoja ilikuwa ni lazima asikilize RTD.

Angalau baadaye, RTD waliunda idhaa nyingine waliyoiita, 'idhaa ya biashara'. Kwa hiyo redio moja ikawa na idhaa mbili 'idhaa ya Taifa na idhaa ya biashara'. Ya taifa ilianza saa 11 alfajiri hadi saa sita usiku inafungwa. Ile ya biashara ilianza saa 10:00 jioni, nafikiri hadi saa nne usiku.

Idhaa ya Taifa ilikuwa ni mambo yote ya msingi, ya Kitaifa, Kimataifa, ikibeba taarifa ya habari, mambo mbalimbali yanayoihusu nchi, kuelemisha wananchi juu ya mambo mbalimbali kama kilimo, afya, uvuvi, kujitegemea na mengine mengine kama utamaduni na maadili. Ni idhaa iliyokuwa ikipiga nyimbo za Kitanzania, zinazopigwa na bendi za Tanzania, au Watanzania wanaoishi nje ya nchi tu basi. Nyimbo za bendi zote za muziki wa dansi nchini zilipigwa hapo. Na za Watanzania waishio nje, zilikuwa kama zile za Simba Wanyika, Les Wanyika na nyingine, ili mradi tu bendi au kundi ni la Watanzania hata kama hawaishi nchini. Pia ilipiga nyimbo za asili kutoka makabila mbalimbali.

Idhaa ya biashara ilikuwa ni maalum kwa ajili ya makampuni, mashirika na taasisi za serikali kutangaza biashara zao hapo. Ndipo tulisikia vipindi kama 'sikiliza bwana umeme', 'benki ya maendeleo vijijini', 'Tasia', 'Tafico', na vingine vingi.

Kwenye idhaa hii sasa, ndipo zilipopatikana hata nyimbo za nje ya nchi. Zilipigwa sana nyimbo za wanamuziki waliotamba sana wakati huo kama Boney M, Jim Reeves, James Brown na wengine wengi.

Ziliruhusiwa pia nyimbo za Afrika Kusini, Kenya na Zaire (sasa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo).

Nyimbo za bendi za Lipua Lipua, Bana Ngenge, Super Mazembe, Les Mangelepa, Shama Shama, Kiam, Veve na zingine. Huko ndiko ilikuwa uwanja wake, lakini haukuweza kabisa kuzisikia kwenye idhaa ya Taifa.

Hebu twende sasa kwenye vipindi ambavyo vilikuwa maarufu sana RTD ambayo aliyekuwa mkubwa, kijana au mtoto wakati huo kuanzia katikati ya miaka ya 1960 hadi katikati ya miaka ya 1990 atakuwa anavikumbuka na atarudisha kumbukumbu zake nyuma.

Baada ya kufunguliwa redio saa 11:00 alfajiri na kufuatiwa na vipindi vya dini, baadaye kinakuja kipindi maarufu kabisa ambacho hakikupendwa kabisa na wanafunzi wa wakati huo, hicho ni 'Kumekucha' hiki kipindi kiliwekwa muda ambao denti wa wakati huo alitakiwa kuamka na kujiandaa kwenda shule.

Baada ya taarifa ya habari ya saa moja, kinafuata kipindi cha 'asubuhi njema' ambacho baadaye kikabadilishwa na kuitwa 'jambo'.

Kuna wakati asubuhi kulikuwa na vipindi vingi vya kawaida, lakini kuanzia saa tatu kuna muda vilikuwa vipindi vya 'shule zetu'. Ilikuwa ni mwendo wa kufundisha tu, kama mwalimu na wanafunzi wako darasani. Hiyo inakwenda hadi saa tano. Hapo unakutana na kipindi cha 'wakati wa kazi'. Wafanyakazi wa taasisi mbalimbali wanahojiwa na kueleza jinsi gani wanavyofanya kazi, kulitumikia taifa, kuwatumikia wananchi na kuzalisha mali.

'Mchana mwema' unafuata, baada ya taarifa ya habari ya saa saba, kuna 'malenga wetu', usisahau pia na kipindi cha 'mashairi', 'shambani', 'vijiji vyetu', 'misitu ni uhai', 'ombi lako' na vingine.

Pia itakumbukwa kulikuwa na vipindi vya 'michezo ya redio', 'Pwagu na Pwaguzi', 'mahoka', 'mazungumzo baada ya habari'. 'Club raha leo show", 'jioni njema', 'mama na mwana', 'harakati', 'kijaluba'.

Vilikuwa vingi sana, lakini sitomaliza kama sijakitaja kipindi cha 'ugua pole'.

Wimbo wa kiashiria cha kipindi hicho ulipigwa na marehemu mwanamuziki Omari Kungubaya.

Mtangazaji alikuwa akienda kwenye hospitali mbalimbali na kuwahoji wagonjwa ambao wanakuwa wamelazwa kwa matatizo mbalimbali. Cha ajabu hata wasomaji ambao walishawahi kuvisikiliza vipindi hivyo ni kwamba wagonjwa wengi waliokuwa wakipewa nafasi ya kuchagua wimbo, walichagua 'Siku ya Kufa' uliopigwa na Orchestra Makassy na kuimbwa na Dk Remmy Ongalla. Kila kipindi ni lazima wimbo huo uombwe, tena na wagonjwa hata nne kwa siku moja.

Na hiyo ilichangia mno wimbo huo kuwa maarufu na kupendwa sana mwanzoni mwa miaka ya 1980 na kuendelea.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

# Ajenda ya siri-24

TINA, msichana kutoka Mpanda, mkoani Katavi anafiwa na wazazi wake wote wawili kwa ajali ya gari akiwa na miaka 10 tu. Tabu alizozipata kutokana na kunyanyaswa na ndugu zake, zilimfanya kuishi maisha ya mateso. Hata shule aliishia la saba tu. Alipofikisha umri wa miaka 18 akakimbilia Dar es Salaam na kuanza kufanya kazi za ndani. Baadaye akabahatika kupata kazi za ndani kwa mfanyabiashara mmoja maarufu, Hafidh Chilambo. Mfanyabiashara huyo anafariki kwa kula chakula kilichowekwa sumu. Chakula hicho kilipikwa na Tina. Mahakama Kuu inamhukumu adhabu ya kunyongwa hadi kufa. Je ni wafanyabiashara wenzake Chilambo ndiyo waliomtuma msichana huyo kwa kumwahidi mamilioni ya pesa kutokana na ugomvi wa kibiashara? Au ni kwa sababu hajalipwa mshahara wake wa miezi sita aliokuwa anadai? Fuatilia kila nakala ya Nipashe ili kuupata ukweli ulio nyuma ya pazia wa sakata hili.

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

MZEE Kalango akasema, Tina Kauzeni aliamka na kufanya kazi zake kama ilivyo siku zote. Ilipofika saa tano asubuhi aliondoka nyumbani hapo. Alirejea baada ya saa moja. Ilipofika saa nane aliondoka tena nyumbani hapo na kwa tajiri yake.

Alimwambia Eddy kuwa nusu saa tu baada ya kuondoka, mke wa marehemu, bi Hellen alirejea nyumbani hapo na ni yeye pekee ndiye aliyemuona.

"Si kweli kwamba alipopeleka watoto wake Temeke kwa shangazi yake hakurejea tena akaenda moja kwa moja kwenye harusi Sinza, alirudi saa tano na nusu asubuhi, akaniambia amerudi mara moja, lakini nisimwambie mtu yeyote yule kama amerudi, si Tina wala mumewe akirejea, lakini hakuniambia wala mimi sikujua kwa nini. Baadaye likatokea tukio hilo, mimi nikaona naitwa napewa pesa nyingi tu, na naambiwa kazi basi, lakini nisiseme kitu chochote kuhusu siku hiyo." Mzee Kalango alimwambia Eddy siku hiyo alipomtembelea Goba.

Akaongeza kuwa mke alionekana amejifungia ndani na hata Tina aliporejea hakujua chochote kama tajiri yake amerudi, na inaonekana alikuwa amejifungia chumbani kwa kufunga na ufunguo kwa ndani, na Tina asingejua chochote, kwani alijua hayupo na chumba kilikuwa kimefungwa. Asingejua kama kuna mtu ndani.

Mahakama ikaendelea kuambiwa kwa ushahidi na vielelezo kutoka kwa mzee Kalango vilivyokusanywa na Eddy kuwa ilipofika saa nane, Tina aliondoka tena, na ndipo mke wa marehemu alipopata tena fursa ya kutoka na kuondoka, akisisitizia mlinzi huyo kuwa asimwambie yeyote kama amerudi, badala yake awaambie hajarudi tangu asubuhi.

"Nilipomuuliza mbona unatoka tena, alimjibu kuwa alipewa ruhusa na mama aende sokoni Ilala kununua nguo na pesa alimpa mwenyewe mama akamwambia ikifika saa nane aende, na saa kumi awahi kurudi kumhudumia mzee chakula. Alipotoka tu na mama naye akatoka ndani na kuondoka, akinisisitizia nisimwambie hata baba kama amerudi."




**Baadaye likatokea tukio hilo, mimi nikaona naitwa napewa pesa nyingi tu, na naambiwa kazi basi, lakini nisiseme kitu chochote kuhusu siku hiyo." Mzee Kalango alimwambia Eddy siku hiyo alipomtembelea Goba.**

Mahakama ilimbiwa Chilambo alianza kula chakula hicho saa 11:00 jioni na baada ya nusu saa alianza kujisikia vibaya, lakini alidhani tumbo tu la kawaida. Chakula hicho kiliandaliwa, kikapikwa na kuwekwa mezani na mshtakiwa Tina Kauzeni.

Upande wa utetezi ukajitetea kuwa ni kweli kiliandaliwa na mtuhumiwa, lakini hakuweka dawa hiyo kwa sababu alimkabidhi Abdallah Mtola. Kijana huyo kwa sasa anaishi humo humo kwenye hiyo nyumba, na ndiyo mara kwa mara anaonekana akitoka kwenye nyumba hiyo na gari hilo la Toyota Alphard.

Upande huo ukadai kuwa ulipopeleleza ulidai kuwa kielelezo kilichopatikana kutoka kwenye hoteli ya Moon Light Sinza kinaonyesha kuwa, mke wa marehemu Chilambo, bi Hellen Kisa aliingia ukumbini saa nne usiku. Itakumbukwa kuwa Eddy Kamal, moja kati ya upelelezi wake na mwisho aliufanya kwenye hoteli hiyo.

Alichofanya kwenda kwenye uongozi wa hoteli na kujitambulisha kuwa ni askari polisi. Alitaka kujua kama tarehe iliyotajwa siku hiyo na mwezi huo kulikuwa na sherehe yoyote kwenye hoteli hiyo.

Akaambiwa ni kweli, kwa mujibu wa kumbukumbu ya vitabu inaonyesha siku hiyo ukumbi wa hoteli uliokodishwa kwa sherehe za harusi, na majina ya wakodishaji yakawekwa wazi.

Akaomba mrejesho wa kamera ya CCTV ya siku hiyo, ili aangalie kabla ya sherehe hiyo ilikuwaje, nani aliingia na saa ngapi.

Kama kawaida, Eddy aliongopa kuwa kuna mhalifu mkubwa aliyefanya uhalifu hapa nchini, lakini anajitetea siku hiyo alikuwa kwenye sherehe za harusi, sasa yeye ametumwa na Jeshi la Polisi kuja kuthibitisha kama alikuwapo au la.

Uongozi ulimruhusu na kamera ikarudishwa nyuma hadi siku ya tukio. Sherehe ikaonekana kuwa ilikuwapo. Nia ya Eddy ni kutaka kuangalia mke wa marehemu Chilambo aliingia saa ngapi siku hiyo.

Kamera ilimuonyesha akiingia saa nne usiku. Alionekana akionyesha kadi ya mwaliko. Alikirekodi kipande hicho na kumkabidhi Tinga kwa ajili ya kukiwasilisha mahakamani. Cha ajabu ni kwamba kipande cha video ya CCTV kilionyesha aliingia yeye na Mtola.

Upande huo wa utetezi ukahoji kuwa kama mke wa marehemu aliondoka nyumbani saa nne ya asubuhi kuwapeleka watoto wake Prisca na Paul kwa shangazi yao Temeke, ili jioni yake aende kwenye sherehe za harusi, kwa nini aliingia ukumbini saa nne usiku? Muda wote huo alikuwa wapi? Na kwa sababu CCTV imemuonyesha akiingia ukumbini saa nne usiku, inakazia maelezo ya mzee Kalango kuwa alirejea nyumbani saa tano na nusu na kujificha chumbani, na hata

Tina aliporejea kununua dawa alizomkabidhi Tinga, yeye mama mwenyewe nyumba alijifungia ndani na hakutaka yeyote ajue kama amerudi, na saa nane alipoondoka mama naye akaondoka, hiyo inatia shaka kuwa lengo lake halikuwa zuri.

Pia, kumtaka mlinzi mzee Kalengo kutomwambia mtu yeyote kama alirudi na akampa pesa nyingi, akimuachisha pia kazi, kinaonyesha kuna kitu alikuwa na nia ya kukifanya, na hakutaka siri ijulikane.

Ushahidi mwingine uliowasilishwa kortini hapo ni ule ambao Eddy aliupata Mbagala Charambe alipokwenda kwa hausiboi wa nyumba ya marehemu, Hussein. Itakumbukwa alimkuta akicheza drafti na baada ya maongezi ya hapa na pale alimpa shilingi elfu hamsini na kufunguka kila kitu.

Hausiboi huyo aliyefanya kazi kwa miaka kumi, alisema anaamini ameondolewa kwa makusudi ili jambo fulani lifanyike.

Na ameshuhudia mambo mengi pale ambayo hayapo, sawa na kubwa zaidi ni kwamba kuna siku aliwakuta Mtola na mama mwenye nyumba wamekumbatiana kimahaba bustanini.


"Nilishtuka sana, na sio siku hiyo tu, siku moja nilidhani mama hayupo, nikaingia ndani, nikawakuta Mtola na mama chumbani katika namna inayoonyesha kabisa ni mtu na mpenzi wake."

Tangu siku hiyo mama alipatwa na wasiwasi mkubwa na akashinikiza mimi niachishwe kazi. Nikaachishwa, lakini baadaye mama akanifuata na kunipa pesa nyingi ili nisiseme chochote. Wale ni wapenzi na si mtu na mjomba wake kama alivyokuwa akidhani marehemu Chilambo." Hussein alimwambia Eddy wakati wa mahojiano.

"Mwanzoni tuliambiwa ni mtu na mjomba wake, alikuwa akija tu na kuondoka, baadaye sana alianza kuwa anakuja na kukaa hata siku tatu nne, au wiki, anaondoka akikaa mwezi, atakuja tena, kila mtu akamzoea mle ndani, mpaka mimi nilipowabamba, lakini sidhani kama Tina na mzee Kalango na wote tuliokuwa tunaishi nao humo tulikuwa tunalitambua hilo, ila ni mimi tu nikaja gundua hilo, peke yangu, wakawa na hofu wakanitimua."

ITAENDELEA JUMAPILI

## HABARI MICHEZO



# RICK ROSS AITAMANI TANZANIA

NYOTA wa muziki wa Hip hop wa Marekani William Leonard Roberts II, maarufu kama Rick Ross, amezidisha joto kwa mashabiki wake baada ya kuelezea nia yake ya kuitembelea Tanzania kwa lengo la kupanda mlima Kilimanjaro.

Akiongea katika Podcast ya FullSend, Rick Ross amesema kuwa amekuwa akisikia mbuga ya wanyama ya Serengeti lakini imefika muda wa kuja kuona mwenyewe.

" Nimekuwa nikipasikia Serengeti kwenye maisha yangu, lakini mpaka kufika hapa miaka 10 ya msoto huko nyuma, imefika muda sasa wa kufurahia maisha yangu na uwezo niliona nao kwa sasa wa kimaisha, nina uwezo wa kwenda kutembea Mlima Kilimajaro," amesema Rick Ross.

# Majizo awatolea uvivu wanaobeza tuzo za Muziki Tanzania

MKURUGENZI mtendaji wa E Media Group, Francis Ciza maarufu Majizzo, amewatolea uvivu wasanii wanaobeza tuzo za muziki , akisema ni hoja za hovyo na hazina uzalendo.

Majizo ameyasema hayo kupitia ukurasa wake wa Instagram, baada ya baadhi ya wasanii kujitokeza na wengine kuonekana hadharani wakizibeza.

Majizzo ameweka wazi kuwa uwepo wa tuzo kwenye tasnia ya muziki ni jambo la muhimu, na zina mchango kwenye tasnia hiyo.

"Tuliokaa kwenye hii game kwa miaka mingi tunafahamu jinsi ambavyo watu walihangaika kuja na tuzo, 'Kili Music Award' zilikuwa tuzo zetu kubwa zaidi, na japo zilikuwa na madhaifu mengi lakini atakuwa mtu wa hovyo sana atakayeshindwa kutambua mchango wa tuzo zile kwenye muziki wetu," amesema.

Majizzo ameongeza kuwa hawezi kutaja majina ya wasanii ambao walivuma wakati wa tuzo hizo na wengine kupata tuzo nyingi.

"Hazikuwa tuzo za kimataifa, ni za hapa ndani, angalau kumbukeni jinsi ambavyo tuzo zilichangamsha game na kufanya watu watoe kazi kali sana," ameongeza.

Akaipongeza serikali kwa kusema "Baada ya muda mrefu wa sisi kutamani tuzo, Serikali yetu imetuletea Tuzo za Muziki Tanzania. Ni kichekesho cha mwaka kusikia kuna wasanii wametukana tuzo hizi na kusema sio lolote. Wamebeza jitihada hizi za Serikali na wadau wengine wa Muziki,"

Hata hivyo amewataka wasanii kuacha tabia ya ubinafsi na kuona hazikua na msaada akiongeza kuwa ni tuzo zilizowainua wasanii wengi na kujenga majina yao.



## ZISIKUPITE

### LACAZETTE ATAKIWA BARCA

BARCELONA inataka kumsajili mshambuliaji wa Arsenal na Ufaransa, Alexandre Lacazette, 30, kwa uhamisho huru mwishoni mwa msimu, mkataba wake utakapomalizika. ***(Sport)***

### TORRES AWINDWA MAN

PAUL Torres, 25, wa Villarreal amerudi kwenye rada za Manchester United ambao msimu uliopita walizungumza na mlinzi huyo wa Hispania kabla ya kuamua kumsajili Raphael Varane. ***(90min)***

### CITY WAKOMAA NA HAALAND

KLABU ya Manchester City ina matumaini ya kuwashinda Real Madrid katika mbio za kumsajili mshambuliaji wa Borussia Dortmund na Norway, Erling Braut Haaland, 21, msimu huu. ***(ESPN)***

### COUTINHO ATAKIWA NEWCASTLE

NEWCASTLE United inataka kumsajili kiungo wa Barcelona na Brazil, Philippe Coutinho, 29, ambaye kwa sasa anacheza kwa mkopo Aston Villa. ***(Sport)***

### OSIMHEN AFUATILIWA ARSENAL

KLABU ya Arsenal imekua ikiwafuatilia kwa karibu mshambuliaji wa Napoli na Nigeria, Victor Osimhen, 23, na mshambuliaji wa Inter Milan na Argentina, Lautaro Martinez, 24. ***(CBS Sports)***

### VILLA NA REKODI

ASTON Villa wanajiandaa kuvunja tena rekodi yao ya usajili msimu huu huenda wakatumia zaidi ya pauni milioni 150 kwa ajili ya kusajili wachezaji wapya. ***(Football Insider)***

### TUCHEL KUMBAKIZA RUDIGER

KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel "ana uhakika" klabu hiyo itaweza kushughulikia suala la mkataba mpya wa mlinzi wa Ujerumani, Antonio Rudiger mwenye umri wa miaka 29. ***(Goal)***

### AARONSON SAFI LEEDS

LEEDS United wako katika nafasi nzuri ya kumsajili kiungo wa Marekani, Brenden Aaronson mwenye umri wa miaka 21, mazungumzo yakiendelea kwa ajili ya uhamisho wake mwishoni mwa msimu akitokea RB Salzburg. ***(Football Insider)***

### SOUCEK HAKIELEWEKI

MAZUNGUMZO kuhusu mkataba mpya wa wa kusalia West Ham kwa kiungo wa Czech, Tomas Soucek, 27, yamesimama hadi mwishoni mwa msimu, licha ya kusakwa na Klabu kubwa Ulaya. ***(90min)***

### CULLEN AWINDWA EPL

WEST Ham na Leeds United ni miongoni mwa klabu zinazotaka kumrejesha England kiungo wa Jamhuri ya Ireland, Josh Cullen, 25, kutoka Anderlecht. ***(Teamtalk)***

### MULLER AANZA MAZUNGUMZO

KLABU ya Bayern Munich imeanza mazungumzo ya mkataba mpya na mshambuliaji wake, Thomas Muller, 32. ***(Bild)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# CAMEROON YAPEWA BRAZIL, TUNISIA KUIVAA UFARANSA

●●● Ni katika droo ya makundi ya kombe la Dunia nchini Qatar 2022, Senegal waangukia kwa Uholanzi...

**DOHA,** Qatar

DROO ya makundi kwa ajili ya michuano ya Kombe la Dunia 2022 nchini Qatar imetolewa, huku wawakilishi kutoka Bara la Afrika wakipewa vigogo vya soka duniani.

**Senegal ipo katika kundi A pamoja na Uholanzi, Qatar na Ecuador, huku Tunisia ikiwa katika kundi D pamoja na Ufaransa, UAE/Australia/Peru na Denmark.**

Cameroon wamepangwa katika kundi G Pamoja na Brazil, Serbia, na Uswisi, huku Morocco ipo katika kundi F pamoja na Ubelgiji, Canada na Croatia.

Wao Ghana wamepangwa kundi H pamoja na Ureno, Uruguay na Korea Kusini. Timu ya taifa ya England imepangwa kundi B pamoja na Iran, Marekani, Scotland/Wales/Ukraine.

Kocha wa England Gareth, Southgate, akizungumziaa droo hiyo katika mahojiano na BBC Sport amesema: "Marekani na Iran ni timu ambazo hatujacheza nazo kwa muda mrefu na ya tatu haijulikani, lakini tutapambana.

"Lazima tutoke nje ya kikundi. Lengo la kwanza ni kutoka nje ya kikundi na kisha tujenge kutoka hapo."

Droo kamili

Kundi A: Qatar, Ecuador, Uholanzi, Senegal

Kundi B: England, Iran, Marekani, Scotland/Wales/Ukraine

Kundi C: Argentina, Saudi Arabia, Mexico, Poland

Kundi D: Ufaransa, UAE/Australia/Peru, Denmark, Tunisia

Kundi E: Hispania, Costa Rica/New Zealand, Ujerumani, Japan

Kundi F: Ubelgiji Canada, Morocco, Croatia

Kundi G: Brazil, Serbia, Uswisi, Cameroon

Kundi H: Ureno, Ghana, Uruguay, Korea Kusini

SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI
PARIS ST GERMAIN
VERSUS
LORIENT
1 | 1.22
X | 6.22
2 | 11.55

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# PEP HANA UHAKIKA HAG KUFANIKIWA MAN UNITED



**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola hana uhakika kama Erik ten Hag atakuwa na mafanikio Manchester United, lakini hana shaka juu ya ubora wa kocha huyo wa Ajax.

Ten Hag anahusishwa na kuhamia United kuchukua nafasi ya Ralf Rangnick, mara baada ya Mjerumani huyo kuacha jukumu lake la muda mwishoni mwa msimu.

Kwa mujibu wa ripoti, Ten Hag alifanya mazungumzo na United katika wiki za hivi karibuni, na hakukanusha uvumi huo katika mahojiano na Sport1 ya Ujerumani.

Kocha huyo mwenye umri wa miaka 52 alisisitiza tena kwamba lengo lake kamili ni Ajax, ingawa aliita United "klabu kubwa yenye mashabiki wakubwa" na kwamba "hakutaka kukataa chochote."

Kocha wa Manchester City, Guardiola alifanya kazi Bayern wakati huo huo Ten Hag alipokuwa akiinoa timu B ya klabu hiyo, na anaamini Mholanzi huyo ana ubora wote wa kufanikiwa katika Ligi Kuu ya England.

Hata hivyo, Guardiola alisisitiza kuwa makocha wengi bora wamekuja na kuondoka United tangu Alex Ferguson alipostaafu mwaka 2013.

Kabla ya pambano la City dhidi ya Burnley jana, Guardiola alisema: "Sijui. Hakuna anayejua. Kama ningekuwa na uhakika kwa asilimia 100, ningewapigia simu Man United, na ningewaambia wanapaswa kumchukua, lakini sijui."



## Apambana kumbakiza Rudiger

**LONDON,** England

THOMAS Tuchel amefichua kuwa 'anajiamini' Antonio Rudiger atasaini mkataba mpya Chelsea, licha ya beki huyo kufanya mazungumzo na Barcelona hivi karibuni.

Mkataba wa sasa wa Rudiger unamalizika mwishoni mwa msimu huu, na 90min inaelewa kuwa ingawa anasubiri matokeo ya kununuliwa klabu, bado kuna uwezekano wa kuondoka kwa uhamisho wa bure katika majira ya joto.

Takriban timu 11 kubwa za Ulaya zimeonesha nia ya kutaka kumnunua mchezaji huyo huku Man Utd, Bayern Munich na Paris Saint-Germain zikiwa miongoni mwa timu zinazowania saini yake.

Barcelona pia wako kwenye kinyang'anyiro hicho huku wababe hao wa LaLiga wameshafanya mkutano wa saa tatu na wawakilishi wa beki huyo wiki hii.

Akihojiwa kuhusu mustakabali wa Rudiger kabla ya mechi ya Chelsea dhidi ya Brentford jana Jumamosi, Tuchel alisisitiza kuwa ana matumaini kuwa The Blues watamfunga kwa mkataba mpya.

CHEZA USHINDE KASINO

JISAJILI CHEZA SHINDA

# JAMHURI, CHIPUKIZI ZAPANDA LIGI KUU Z'BAR

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Jamhuri na Chipukizi zimepanda daraja na zitacheza ligi Kuu ya Zanzibar msimu ujao wa 2022/2023.

Jamhuri na Chipukizi zimefanikiwa kupanda daraja baada ya juzi kushinda katika mchezo wa 'play off' kwenye ligi daraja la Kwanza Kanda ya Pemba.

Jamhuri iliifunga New stone Town 1-0, wakati Chipukizi waliibuka na ushindi mnono wa 4-1 didi ya Hard Rock.

Jamhuri na Chipukizi zimerudi Ligi Kuu baada ya kushuka daraja msimu uliopita wa 2020-2021.

**Wakati Kisiwani Pemba tayari ligi daraja la Kwanza Kanda imemalizika, lakini kwa upande wa ligi daraja la Kwanza Kanda ya Unguja imebakisha michezo 10 ili kuzipata timu mbili zitakazoungana na timu za kanda ya Pemba kucheza ligi Kuu msimu ujao.**

Akizungumza na gazeti hili, Mwenyekiti wa Bodi ya Ligi ya Zanzibar, Haji Kidali alisema kuchelewa kumalizika kwa ligi daraja la Kwanza Kanda ya Unguja kumetokana na kusimama kwa vipindi viwili.

Alisema ligi ya Kanda ilisimama wakati wa michuano ya kombe la Mapinduzi ambapo Pemba iliendelea, lakini pia katika kipindi hiki cha mfungo wa Ramadhani pia itasimama.

Aidha Bodi ya Ligi imezipongeza timu hizo kwa jitahada zao na kurudi ligi kuu, lakini pia alizitaka zihakikishe zinafuata matakwa ya leseni ya klabu.



Wachezaji wa timu ya Wanawake inayolelewa na Kituo cha Jakaya Kikwete (JMK), wakiwania mpira wakati walipokuwa wakifanya mazoezi katika viwanja vya Kituo hicho jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Simbu, Natalie ndani ya mbio za kimataifa leo*

**Na Cheji Bakari,** TANGA

WANARIADHA Alphonce Simbu na Natalia Elisante Sulle leo Jumapili watashiriki mashindano ya riadha ya kimataifa nchini Italia na Korea Kusini.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Chama cha Riadha (RT), Simbu atakuwa jijini Milan nchini Italia ambapo atashiriki katika mbio za Milan International Marathon na Natalia atashiriki kukimbia mbio za Daegu International Marathon nchini Korea Kusini.

Simbu na Natalie ni miongoni mwa wanariadha wa timu ya Taifa ya Riadha ambayo inatarajiwa kuiwakilisha nchi kwenye mbio za Jumuiya ya Madola zitakazofanyika Agosti mwaka huu nchini England.

Katika hatua nyingine, wachezaji wanne wa mbio fupi wa timu ya Taifa ya Riadha ambao walikuwa wameweka kambi ya mwezi mmoja eneo la West Kilimanjaro mkoani Kilimanjaro wamehamishiwa katika kambi ya hosteli za Jeshi la Wokovu, Mgulani jijini Dar es Salaam.

Wachezaji hao ni Ainess Johnson,Ally Gulamu,Winifrida Makenji na Elias Turan.

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 03/04/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:15 | 4385 | PEC Zwolle vs GO Ahead Eagles | 2.01 | 3.32 | 3.56 |
| 13:30 | 1355 | Kasimpasa vs Gaziantep BB | 2.04 | 3.53 | 3.33 |
| 13:30 | 5343 | Fiorentina vs Empoli | 1.52 | 4.40 | 5.40 |
| 14:00 | 1421 | FC Krasnodar vs Dinamo Moscow | 3.37 | 3.37 | 2.05 |
| 14:00 | 3528 | Rangers vs Celtic | 2.41 | 3.24 | 2.84 |
| 14:00 | 5398 | Strasbourg vs Lens | 2.11 | 3.31 | 3.46 |
| 14:30 | 1364 | Standard Liege vs Union Saint Gilloise | 4.68 | 3.74 | 1.68 |
| 15:00 | 5280 | Athletic Bilbao vs Elche | 1.46 | 4.24 | 7.07 |
| 15:15 | 3569 | FC Luzern vs FC Lugano | 2.28 | 3.20 | 3.10 |
| 15:30 | 3491 | Fortuna Sittard vs Heracles Almelo | 2.58 | 3.28 | 2.58 |
| 15:30 | 4234 | Sparta Rotterdam vs Heerenveen | 2.17 | 3.13 | 3.33 |
| 16:00 | 2652 | Udinese vs Cagliari | 1.81 | 3.51 | 4.32 |
| 16:00 | 3243 | Konyaspor vs Goeztepe | 1.86 | 3.58 | 3.88 |
| 16:00 | 3925 | Clermont Foot vs Nantes | 2.55 | 3.05 | 2.90 |
| 16:00 | 4047 | Troyes vs Reims | 2.56 | 2.96 | 2.96 |
| 16:00 | 4341 | Sirius FK vs GIF Sundsvall | 1.71 | 3.64 | 4.17 |
| 16:00 | 4527 | West Ham vs Everton | 1.76 | 3.65 | 4.40 |
| 16:00 | 4656 | Alanyaspor vs Caykur Rizespor | 1.65 | 3.89 | 4.69 |
| 16:00 | 4707 | Montpellier vs Brest | 2.10 | 3.43 | 3.38 |
| 16:00 | 5549 | Atalanta vs Napoli | 2.36 | 3.25 | 2.95 |
| 16:00 | 5689 | Metz vs Monaco | 6.03 | 4.02 | 1.54 |
| 16:30 | 3361 | CSKA Moscow vs Ural Yekaterinburg | 1.40 | 4.27 | 7.55 |
| 16:30 | 3608 | Augsburg vs VfL Wolfsburg | 2.84 | 3.24 | 2.45 |
| 17:00 | 1772 | Cercle Brugge vs KAA Gent | 3.23 | 3.38 | 2.13 |
| 17:15 | 4062 | Betis vs Osasuna | 1.99 | 3.44 | 3.74 |
| 17:30 | 2181 | Maritimo vs Tondela | 2.06 | 3.35 | 3.45 |
| 17:30 | 4225 | FC Basel vs BSC Young Boys | 2.85 | 3.64 | 2.23 |
| 17:45 | 5537 | Cambuur vs NEC Nijmegen | 2.43 | 3.41 | 2.67 |
| 18:00 | 5593 | Cape Town City vs Baroka FC | 1.76 | 3.40 | 4.80 |
| 18:05 | 3964 | Lyon vs Angers | 1.38 | 4.81 | 7.42 |
| 18:30 | 1830 | Monchengladbach vs Mainz | 2.22 | 3.50 | 3.00 |
| 18:30 | 2912 | Kalmar vs Malmo | 4.38 | 3.55 | 1.69 |
| 18:30 | 2917 | Norrkoping vs Varbergs Bois | 1.56 | 3.91 | 4.89 |
| 18:30 | 3011 | Tottenham vs Newcastle | 1.49 | 4.30 | 6.00 |
| 19:00 | 3000 | Sampdoria vs Roma | 3.96 | 3.56 | 1.86 |
| 19:00 | 4994 | Sochi vs Zenit St Petersburg | 3.82 | 3.67 | 1.83 |
| 19:00 | 5658 | Jerv vs Stromsgodset | 2.49 | 3.33 | 2.68 |
| 19:30 | 1114 | Anderlecht vs Charleroi | 1.48 | 4.40 | 5.80 |
| 19:30 | 5042 | Granada vs Rayo Vallecano | 2.61 | 3.11 | 2.81 |
| 19:30 | 5349 | Valencia vs Cadiz CF | 1.86 | 3.37 | 4.43 |
| 20:00 | 4193 | Moreirense vs Vitoria Guimaraes | 2.88 | 3.18 | 2.42 |
| 20:00 | 4902 | Viktoria Plzen vs Slavia Prague | 3.03 | 3.23 | 2.38 |
| 20:30 | 1982 | Trabzonspor vs Besiktas | 2.11 | 3.43 | 3.23 |
| 21:00 | 3598 | Bodo Glimt vs Rosenborg | 1.51 | 4.29 | 5.59 |
| 21:45 | 2314 | Juventus vs Inter | 2.77 | 3.22 | 2.51 |
| 21:45 | 4834 | Paris St Germain vs Lorient | 1.22 | 6.22 | 11.55 |
| 22:00 | 2880 | Racing Genk vs Eupen | 1.40 | 4.77 | 6.56 |
| 22:00 | 3626 | Barcelona vs Sevilla FC | 1.54 | 4.08 | 6.07 |
| 22:30 | 4575 | Sporting Lisbon vs Pacos Ferreira | 1.21 | 5.80 | 13.01 |
| 23:30 | 1557 | Portland Timbers vs LA Galaxy | 2.22 | 3.50 | 3.09 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumapili Aprili 3, 2022

Ni e



Tuchel apambana kumbakiza Rudiger UKURASA 22



Wachezaji wa Simba (kutoka kushoto) Joash Onyango, Peter Banda, Shomari Kapombe na Bernard Morris wakiwa kwenye mazoezi kujiandaa na mchezo wa Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya US Gendermerie ya Niger, utakaopigwa leo uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam. **PICHA: SIMBA**

# SIMBA KUSUKA AU KUNYOA LEO

## Ni katika mchezo wa Kombe la Shirikisho dhidi ya Gendermerie ambao...

**Na Adam Fungamwango**

NI kusuka au kunyoa leo kwa wawakilishi wa Tanzania kwenye michuano ya kimataifa, Simba wanaotakiwa wapate ushindi wa aina yoyote ile dhidi ya US Gendermerie ya Niger ili kutinga hatua ya robo fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika.

**Mechi hiyo inachezwa majira ya saa nne usiku kwa saa za Afrika Mashariki, ikicheza pamoja na mechi kati ya RS Berkane ya Morocco dhidi ya Asec Mimosas ya Ivory Coast ili kuondoa uwezekano wa kupanga matokeo, lakini kwa saa za Morocco itakuwa ni saa mbili usiku.**

Itakuwa ikicheza mbele ya mashabiki wake wapatao 35,000 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa ambao umekuwa ukiwapa ushindi kwa asilimia nyingi pale kwenye mechi za kuamua.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Pablo Franco amesema wachezaji wake wako katika hali nzuri ya kupambania timu na Tanzania kwa ujumla kwa ajili ya kuhakikisha matokeo mazuri yanapatikana.

"Nafahamu ugumu tutakaokutana nao kwa sababu US Gendermerie siyo timu ya mzaha, lakini niwaondoe hofu mashabiki wa Simba, kwani wachezaji hawatobweteka, kila mmoja anatakiwa kupambana ili kutimiza ndoto ya kutinga hatua hiyo," alisema kocha huyo ambaye kikosi chake kilitoka sare ya bao 1-1 ugenini dhidi ya timu hiyo Februari 20 mwaka huu kwenye Uwanja wa Jenerali Seyni Kountche nchini Niger.

Juzi, Rais wa Heshima wa klabu hiyo, Mohamed Dewji aliwatembelea kambini wachezaji wa timu hiyo na kuongea nao, kuongeza bonasi ili kuwafanya wapambane kwa ajili ya kufanikisha ushindi ambao licha ya kuifanya Simba kutinga hatua ya robo fainali, utaifanya Tanzania kupeleka moja kwa moja timu nne kwenye michuano ya kimataifa msimu ujao.

Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, naye wiki nzima amekuwa kwenye pilikapilika ya kuhamasisha mashabiki kuelekea kwenye mechi hiyo, pamoja na kujumuika na wanachama na mashabiki wa timu hiyo kwenye stendi ya Magufuli maeneo ya Mbezi Louis, ambapo vikundi mbalimbali vya ngoma kutoka matawi kadhaa Dar es Salaam na Pwani, vilikutana.

Kuelekea kwenye mechi hiyo, pia alifanya ziara ya kupanda treni ya reli ya kati kutoka Dar es Salaam hadi Pugu na kurejea tena, ambapo akiwa ndani alipata fursa ya kuzungumza na mashabiki kwa ajili ya kuwahimiza wajitokeze na kuwapa hamasa wachezaji.

Alijumuika pia na wasanii wa bongo fleva na filamu ambao ni wanachama na mashabiki wa timu hiyo kwa ajili ya kuamsha hamasa.

Simba inakamata nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Kundi D kwa pointi saba na inahitaji ushindi ili kwenda robo fainali na timu yoyote itakayoshinda kati ya RS Berkane au Asec Mimosas, kwani itakuwa na pointi 10.

# Yanga yanoa fowadi, Azam FC mabeki

**Na Saada Akida**

WAKATI Yanga wakihakikisha safu ya ushambuliaji inakuwa imara, Azam FC nao wanapanga vema beki zao ili kuhakikisha hawatoi nafasi kwa mastraika wa wapinzani wao kutikisa nyavu, kwenye mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Yanga watakuwa ugenini katika mchezo huo utakaopigwa Aprili 6, mwaka huu katika uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi nje kidogo ya Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze alisema wanaendelea na maandalizi ya mchezo wao dhidi ya Azam FC na kuhakikisha wanaendelea kupata matokeo mazuri.

Alisema ameona Azam inavyocheza ina wachezaji wazuri, pia wanatarajia kuingia na mfumo tofauti ikiwemo kutumia washambuliaji wawili katika mchezo huo.

"Mchezo utakuwa wa ushindani mkubwa kulingana na wapinzani wetu ni wazuri, tunatarajia kuingia na mfumo tofauti ikiwezekana kutumia washambuliaji wawili, katika mchezo huo kuhakikisha tunapata pointi muhimu," alisema Kaze.

Alisema kutokana na ushindani na ugumu wa mchezo huo wanatarajia kutumia washambuliaji wawili hali ambayo inawalazimu kujenga kombinesheni kati ya Fiston Mayele na Heritier Makambo.

"Tumekuwa tukijaribu kufanya hivyo katika mazoezi yetu na hata mechi zetu za kirafiki kuwapa mbinu washambuliji wetu kuendelea kupata matokeo mazuri katika mchezo huo," alisema Kaze.

Naye Kocha wa Azam, Moallin alisema amewaona Yanga na anawaheshimu na ataingia kwa tahadhari kubwa kuhakikisha hawapati nafasi ya kupata pointi tatu.

9 770856 541002 >